# Nipashe

Jumamosi Februari 1, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581939

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


**MITAMBO** minane Bwawa la Nyerere yawashwa rasmi, mwingine Februari

UKURASA 2



**WAKUU** SADC walaani mapigano DR Congo



UKURASA 2

**WAFARIKI** dunia madai ya kunywa pombe kali, polisi yazuia kuzikwa

UKURASA 5

# Mimba 200,000 zaharibika mwaka 2024

**WAZIRI:** Baadhi wanaozitoa si za waume zao, waigharimu serikali mabilioni kwenye matibabu Endelea Ukurasa wa 3



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Gowin Mollel, akijibu maswali bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wanaojifungua watoto njiti sasa kicheko, wadau wafurahia

UKURASA 4

UKURASA WA 8

## 'FICHUENI WAKOPESHAJI WA MIKOPO UMIZA'

WAJASIRIAMALI na wananchi wa Wilaya ya Monduli mkoani Arusha,..

UKURASA WA 24

## YANGA YAWAAHIDI FURAHA MASHABIKI

WAKATI inatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania...

## BUNGE LAPITISHA AZIMIO KUMPONGEZA RAIS SAMIA MKUTANO NISHATI AFRIKA

UKURASA 2



Wafanyabiashara wa Soko la Samunge, jijini Arusha wakifunga barabara ya Samunge-Fire jana, kuishinikiza serikali kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwamo mgambo wa eneo hilo, kukamata bidhaa zao licha ya kulipa ushuru kila siku, chemba za vyoo kuziba na kusababisha majitaka kusambaa kwenye sehemu zao za biashara. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

MICHEZO SIMBA: TUNAKWENDA TABORA KULIPIZA KISASI UK. 24

KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA

## Mradi Bwawa la Nyerere kukamilika Februari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere utakamilika rasmi mwishoni mwa Februari, mwaka huu, baada ya kukabidhiwa mtambo wa tisa wa kuzalisha umeme.

Akichangia jana bungeni azimio la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa nishati Afrika, Dk. Biteko alisema bwawa hilo lilipaswa kukamilika ifikapo Mei mwaka huu.

"Hadi leo asubuhi mitambo yote minane imekabidhiwa na mtambo mmoja, ambao ni wa tisa, utakabidhiwa mwishoni mwa Februari, mwaka huu, na mradi wa bwawa hili tutakuwa tumemaliza," alisema.

Dk. Biteko pia alisema mpango wa nishati umetoa viashiria vitano kikiwamo cha upatikanaji wa umeme kwa Tanzania kwa asilimia 78.4.

Alisema katika mpango huo walitia saini miaka mitano ijayo Tanzania itafikia upatikanaji wa umeme kwa asilimia 100.

"Uunganishaji umeme na wateja leo tunapozungumza hatua tuliyo nayo, tumeunganisha wateja milioni 5.5 na mpango ni kupeleka kwa wateja milioni 13.5 na usingekuwa mpango huo wangepambana na wasingezidi milioni 5.2," alisema.

Alisema kuwa kwenye nishati safi ya kupikia wanataka watoke asilimia 9.9 kwenda asilimia 75 ndani ya miaka mitano.

"Mchango wa nishati jadidifu itoke asilimia 56 iliyopo twende asilimia 65 na tutalifikia suala hili bila wasiwasi wowote," alisema.

Biteko alisema mkutano huo ulikuwa na mwitikio mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia. "Sababu mbili zilizofanya mkutano huu kuja Tanzania ni kuimarika kwa diplomasia yetu na mataifa mengine na haijaimarishwa na mwingine ni yeye Rais Samia. Kasi kubwa ya upelekaji umeme kwa wananchi hasa vijijini, Benki ya Dunia walivyofanya tathmini mwaka jana Tanzania iliongoza na wakaona mahali pekee pakupeleka mpango huu ni Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa Rais Samia ametoa msukumo mkubwa kwenye sekta ya nishati na kuahidi makubaliano yaliyofikiwa kwenye mkutano huo atayasimamia na hayatabaki kwenye makaratasi.

Naye Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alipongeza serikali kwa kukamilisha mradi wa Nyerere kabla ya muda uliopangwa na kwamba fedha zilizokuwa zinaelekezwa kwenye masuala ya umeme sasa zitapelekwa miradi mingine ikiwamo barabara ambazo wabunge wamekuwa wakipigia kelele.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Robert Mugabe, jijini Harare, Zimbabwe jana, kwa ajili ya kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jana. **PICHA: IKULU**

# Bunge lapitisha azimio kumpongeza Rais Samia Mkutano Nishati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (Mission 300) Mwaka 2025 kwamba, umeiletea sifa ya kipekee Tanzania na kutaja namna Watanzania walivyonufaika.

Akisoma azimio la pongezi hizo bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asia Halamga, alisema mkutano huo ulikuwa na manufaa makubwa kwa uchumi wa Tanzania na Bara zima la Afrika.

Alisema wawekezaji katika sekta ya hoteli na malazi, usafiri na usafirishaji, wauzaji wa vyakula na vinywaji, wauzaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na sekta ya utalii wamenufaika na Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

"Kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano, wafanyabiashara wameweza kutengeneza mtandao katika biashara zao kwa kufanya mazungumzo ya kibiashara, yaani Business to Business na Business to Customer (B2B na B2C) pembezoni mwa mkutano huo na tumeingiza fedha za kigeni, suala ambalo limeleta manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu," alisema.

Alisema mkutano huo umeazimia masuala mbalimbali yakiwamo mataifa mbalimbali yametoa ahadi za mipango ya mageuzi makubwa ya nishati yanayolenga kuimarisha nishati mbadala na jadidifu, kuboreshwa kwa gridi za umeme na kuimarisha upatikanaji wa suluhu ya nishati safi za kupikia.

Pia alisema kuzinduliwa kwa Mipango ya Kitaifa ya Nishati kwa lengo la kuvutia wawekezaji na mageuzi ya sera; kutolewa kwa ahadi za ufadhili kutoka taasisi za kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia.

Alisema kuvutia sekta binafsi kuwekeza mitaji katika sekta ya nishati barani Afrika na kufikiwa kwa Azimio la Dar es Salaam, ambalo limelenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030.

"Azimo la Dar es Salaam linamanufaa makubwa kwa Bara la Afrika, kwani kupitia azimio hilo, imekubalika kwamba, upo umuhimu wa kuzingatia usawa wa kijinsia katika kuongeza upatikanaji wa nishati hasa kwa wanawake na wafanyakazi, ili kuimarisha muhstakabali endelevu,"alisema.

Vilevile, azimio hilo linasisitiza umuhimu wa kuunganisha nishati kati ya nchi za Afrika, kutumia vyanzo vya nishati jadidifu kama jua, upepo, umeme wa maji, nishati za joto ardhi, ili kuwa na mifumo imara ya nishati.

Alisema wanampongeza Rais Samia kwa mafanikio hayo na kuhudhuriwa na wageni takribani 2,600 wakiwamo wakuu wa serikali na nchi takribani 21 kutoka barani Afrika, mawaziri na viongozi mbalimbali wa taasisi za kimataifa za fedha na nishati na wadau wengine.

Mbunge huyo alisema mkutano ulikuwa wa weledi na viwango vya hali ya juu kimataifa kutokana na uratibu mzuri uliofanywa na serikali anayoiongoza.

"Rais Samia ameonesha nia ya dhati kuhakikisha kuwa ifikapo 2030, asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia 2034, Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia," alisema.

**KISHOA AGUSWA**

Akichangia azimio hilo, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Jesca Kishoa, alisema anaungana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa uamuzi wa kumpitisha Samia kuwa mgombea urais katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, mwaka huu, kwa maono aliyo nayo kwenye nishati, uchumi na diplomasia.

Alisema Rais Samia amefanya kazi ya kuimarisha diplomasia, uchumi na kuwa kinara wa matumizi ya nishati safi.

"Kwa haya yaliyofanyika mkutano mkuu na mengine haya mambo yamehalalisha uamuzi wa mkutano mkuu wa CCM yaliyofanyika mwaka huu na mimi ninaungana kwa asilimia 100 kwa uamuzi wa wajumbe wa CCM walioufanya," alisema.

# Wakuu wa SADC walaani mapigano DRC

**Na Restuta James**

WAKUU wa nchi na serikali kutoka Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), wamelaani vita vinavyoendelea Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) huku wakisisitiza dhamira yao ya kuhakikisha usalama na amani ya kikanda.

Viongozi hao waliitisha mkutano wa dharura jana Harare, Zimbabwe, kwa lengo la kujadili hali ya usalama katika eneo hilo.

Mkutano huo uliongozwa na Rais wa Zimbabwe na Mwenyekiti wa SADC, Dk. Emmerson Mnangagwa, ambaye katika hotuba yake ya ufunguzi, alisisitiza haja ya dharura ya kuimarishwa kwa juhudi za kujenga amani na mazungumzo ili kutatua mgogoro huo.

Alisema jukumu la SADC ni kujitolea kulinda amani na usalama wa kikanda na kuahidi kuongeza juhudi za kulinda raia kutokana na kukosekana kwa utulivu kwa mujibu wa Mkataba wa Ulinzi wa Pamoja wa SADC.

Rais Mnangagwa alisisitiza umuhimu wa kuimarisha utashi wa kisiasa katika eneo lote, kwa lengo la kutengeneza mkakati unaotekelezeka wa kuleta amani Mashariki mwa DRC.

Alishukuru juhudi za washirika wa kimataifa kuhusu mzozo huo na kusisitiza kuwa kazi kubwa zaidi inahitajika kufanywa ili kupunguza mateso ya watu waliokimbia makazi katika eneo hilo.

"Mzozo unaoendelea Mashariki mwa DRC, unaotokana na migogoro ya silaha inayoendelea, hauwezi kupuuzwa. Watu wa eneo hili wameteseka kwa muda mrefu sana," Mnangagwa alisema.

Mkutano huo uliwakutanisha wakuu wa nchi kutoka nchi kadhaa wanachama wa SADC. Viongozi hao walionesha mshikamano usioyumba na watu wa mashariki mwa DRC na kusisitiza kujitolea kwao kutafuta suluhu za kudumu kwa ghasia zinazoendelea.

Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) alikuwa miongoni mwa wakuu wa nchi wanaoshiriki kikao hicho muhimu.

Aidha, Rais Felix Tshisekedi alihudhuria mkutano huo kwa mtandao.

Lengo kuu la mkutano huo wa dharura lilikuwa kuandaa mkakati wa kina wa amani, kutumia ushirikiano wa kikanda na msaada wa kimataifa, ili kurejesha amani ya kudumu na utulivu katika eneo lenye matatizo.

Katibu Mtendaji wa SADC, Elias Magosi, alisema kutokana na uzito wa hali ya usalama Mashariki mwa DRC, mkutano huo umeitishwa ili kutathmini na kuimarisha mwitikio wa pamoja wa amani na usalama nchini humo.

"Majadiliano katika mkutano huu yanathibitisha dhamira isiyoyumba ya SADC ya kusaidia DRC na kuhakikisha utulivu wa muda mrefu katika kanda.

"Nina imani kwamba uamuzi uliyofanywa hapa utaakisi mshikamano wetu unaoendelea na watu wa DRC na dhamira yetu pana ya kuimarisha usalama na utulivu katika eneo lote na bara.

"Ukanda wetu umejulikana kwa muda mrefu kwa kuishi kwa amani na ustahimilivu. Imesalia kuwa ni mwanga wa matumaini kwa watu wa SADC na Afrika kwa ujumla, hasa katika ulimwengu ambao wengi wanaendelea kustahimili athari mbaya za migogoro na ukosefu wa utulivu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Zaidi ya mimba 200,000 zaharibika mwaka 2024

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema kwa mwaka 2024 iliwapokea na kuwapa huduma jumla ya wanawake na wasichana 213, 675 waliopata changamoto ya kuharibika kwa ujauzito nchini.

Vilevile, serikali imeliarifu Bunge kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022 hadi 2024, wanawake 92 walipoteza maisha kutokana na changamoto mbalimbali zilizosababishwa na kuharibika kwa ujauzito.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, aliyetaka kujua idadi ya wasichana na wanawake walioathirika na utoaji mimba usio salama nchini.

Akijibu swali la mbunge huyo, Dk. Mollel alibainisha kuwa kati ya wagonjwa 213,675 waliopatiwa matibabu baada ya ujauzito kuharibika mwaka 2024, wasichana 181, 071 walipatiwa huduma na kuruhusiwa kama wagonjwa wa nje na 32,512 walipatiwa huduma wakiwa wamelazwa.

Takwimu rasmi za Wizara ya Afya zinaonesha kuwapo wastani wa wanawake milioni mbili wanaoshika ujauzito kila mwaka, wakijifungua watoto milioni 2.4 (baadhi yao hujifungua watoto pacha).

**MIMBA ZA KUBAKWA**

Mbunge Fatuma pia alitaka kauli ya serikali kuhusu wanawake wanaobakwa na kupata mimba zisizotarajiwa.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema kuna haja kutoa elimu ya saikolojia kwa wasichana na wanawake wanaopitia kadhia hiyo na kuhakikisha jamii inapewa elimu vya kutosha ili kuepuka tabia hizo kujitokeza.

"Sisi tuwe mabalozi kwenye jamii kuhakikisha eneo hili la wanawake kunyanyaswa na kubakwa hayatokei kwenye jamii yetu," alisema Dk. Mollel pasi na kutaja idadi ya wanaokumbwa na ukatili huo nchi, kama ilivyohojiwa na mbunge.

Alisema serikali imekuwa na mkakati endelevu wa kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa jamii na kusogeza huduma karibu na wananchi. Mpaka sasa imeshajenga zaidi ya vituo 480 ili kurahisisha upatikanaji huduma hiyo.

Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Tea Ntala, alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha kuwa matumizi ya dawa za kuzuia kupata ujauzito, maarufu P2, yanaelezwa vizuri ili wasichana wasiathirike ikiwamo kukosa watoto.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali imeshaanzisha kampeni maalum iliyopewa jina la 'Holela Holela Itakukost' iliyolenga kutoa elimu kuhusu matumizi mabaya ya dawa, zikiwamo P2.

Aliwaomba wabunge kuendelea kuhimiza kuhusu matumizi mabaya ya dawa, zikiwamo P2, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Kenan, alihoji kama serikali imefanya tathmini ya kugundua kiini cha utoaji mimba usio salama.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema suala hilo linasababishwa na kutokuwa na elimu na linaigharimu serikali kwa sababu wengi wanazitoa, wanafikishwa hospitalini wakiwa na hali mbaya na hawana fedha za matibabu, hivyo wanatibiwa pasipo kulipia.

Alisema kuna haja kutoa elimu kuanzia shule za msingi na kuendelea kuhusu madhara ya utoaji mimba.

Naibu Waziri Mollel alidokeza lingine la ziada kwamba wakati mwingine wanawake walioolewa wamekuwa wanatoa mimba wanapogundua kuwa siyo za waume zao.

"Lakini pia wakati mwingine kinamama inatokea amebeba mimba ambayo anajua siyo ya mume wake na inatokea mambo kama hayo (anaitoa)," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Felister Njau, alihoji lini serikali itakuja na sheria ya kumlinda mwanamke ambaye amepata mimba isiyotariwa kama vile kubakwa na ndugu.

Katika majibu yake kwa swali hilo, Dk. Mollel alisema sheria za kumlinda mwanamke anayepitia kadhia hiyo zipo ila kuna haja ya kuelimisha jamii ili kuongeza uadilifu, utu na upendo. Itasaidia kuepuka "majanga kama hayo".



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (wa pili kulia), akizungumza na baadhi ya wakulima wa zao la pamba katika kijiji cha Kisuke, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama juzi, wakati wa ziara yake ya kukagua kilimo cha zao hilo. **PICHA: SHABAN NJIA**

## RC ashangaa nyaraka za ushirika kuhifadhiwa kwenye jaba la maji

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, ameonesha kushangazwa na uhifadhi holela wa nyaraka za wakulima wa pamba katika Chama cha Msingi (AMCOS) Kata ya Kisuke Halmashauri ya Ushetu.

Macha amepata mshangao huo baada ya kubaini kuwa nyaraka hizo kuwa katika jaba la kuhifadhia maji, huku kukiwa hakuna taarifa ya mapato, matumizi na uzalishaji wa zao hilo.

Aliyabaini hayo jana baada ya kumtaka mwenyekiti wa chama hicho, Cosmas Shija, kumpatia taarifa ya hali ya uzalishaji wa pamba, idadi ya wakulima alio nao, pembejeo na viwatilifu alivyopokea na kukuta nyaraka hizo zinahifadhiwa kwenye jaba la maji na kutelekezwa kwenye ghala la pamba.

Shija alisema wanahifadhi nyaraka muhimu za wakulima wa zao hilo kwenye jaba la maji na kuliweka kwenye ghala la pamba kwa sababu ya kukosa mahala salama pakuzihifadhi.

Alisema hawana taarifa ya mapato na matumizi kwa sababu ya mapato yao kushuka tangu Agosti, mwaka jana.

"Ni kweli nyaraka zetu tunazihifadhi kwenye jaba la maji ambalo lipo ndani ya ghala la kuhifadhi pamba. Hatuna taarifa ya mapato na matumizi kwa sababu mapato yetu yameshuka tangu mwaka jana tulipopata Sh. 200,000 na tukashindwa kutengeneza ofisi ya kuhifadhi nyaraka," alisema Shija.

Katibu wa chama hicho, Letisia Daudi, alisema walipokea tani 6.5 za mbegu na kuzigawa kwa wakulima 135 kwa uwiano sawa na kila mmoja amelima zao hilo ekari moja na kuendelea na hivi karibuni wamepokea mabomba 30 yanayotumika kupulizia dawa shambani ili kuua wadudu wanaoshambulia mimea.

Kutokana na hali hiyo, Macha aliwataka viongozi hao kuandaa taarifa ya hali ya uzalishaji wa pamba, pembejeo na viwatilifu walivyopokea pamoja na taarifa ya mapato na matumizi kwa kushirikiana na ofisa kilimo wao wa kata na kuikabidhi kwa mkuu wa wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, na kuacha kujificha kwenye mwavuli wa kushuka kwa mapato.

Hata hivyo, Macha aliwaahidi kuwapatia viti na meza vyenye uwezo wa kuhifadhi nyaraka za wakulima na kuachana na kuhifadhi kwenye jaba pamoja na kufanya vikao mara kwa mara ili kuwasikiliza wakulima na kuwasilisha changamoto zao katika bodi ya pamba na kutafutiwa ufumbuzi.

Pia aliwataka kuwatumia maofisa kilimo wa vijiji na kata katika kuwaelimisha namna sahihi ya kulima kisasa kwa kuzingatia kanuni 10 bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji na kundokana na kupata kilo 300 mpaka 500 kwa ekari mpaka kilo 1,200 na kujipatia kipato.

## Mchakato wa utoaji fedha miundombinu afya, elimu waiva

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI iko katika hatua za mwisho za kutoa fedha kwa ajili ya vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo na ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa na wananchi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema jana bungeni jijini hapa wakati akitoa majibu ya nyongeza baada ya maswali ya wabunge kuhusu fedha za ujenzi wa vituo vya afya na ukamilishaji wa maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi katika sekta za afya na elimu.

"Tuko katika hatua ya mwisho kuanza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya elimu na vituo vya afya msingi itakayokwenda sambamba na ukamilishaji wa maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu ya wananchi," alisema.

Awali Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba, alilieleza Bunge kuwa serikali itatoa Sh. milioni 250 kwa kila jimbo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya kutolea huduma za afya msingi, zikiwamo zahanati.

Alisema wabunge walijaza fomu za kuainisha maeneo ya kimkakati katika majimbo yao ili kujenga vituo vya afya kupitia fedha kutoka Serikali Kuu na mapato ya ndani kutoka halmashauri.

Aidha, alizihimiza halmashauri kupitia mapato ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo muhimu ya afya msingi.

# Dawa wanaozuia maiti kisa deni sasa yamcheka

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imesema itaanza kuchukua hatua kali kwa madaktari wanaozuia mwili kuchukuliwa na ndugu zao baada ya kushindwa kulipa gharama za matibabu, kinyume na maelekezo ya serikali.

Kadhalika, imetoa maelekezo kwa hospitali binafsi na za umma kuhakikisha wanatoa kwanza huduma kwa wagonjwa na si kuweka maslahi ya fedha mbele.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati akijibu swali la Mbunge wa Segerea, Bonnah Kamoli, lililokuwa likiuliza serikali inatoa tamko gani la wazi kwa wananchi wanaoshindwa kupata mwili kwa baada ya kushindwa kulipa deni.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema serikali imekuwa ikipokea malalamiko ya ndugu kuchelewa kupewa miili kwa kushindwa kulipa madeni.

Dk. Mollel alisema kutokana na hilo, serikali itachukua hatua kwa daktari atakayesababisha usumbufu kama huo, ikiwa mwananchi anafuata taratibu zinazohitajika.

Alisema serikali ilishatoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Waraka Namba Moja wa Mwaka 2021 wa kutozuia mwili na kuweka utaratibu wa kulipia gharama za matibabu na madeni ya miili.

Naibu Waziri aliwaomba wabunge kuwaelimisha wananchi wao kufuata taratibu watakazopewa pale wanaposhindwa kulipa deni, kuwapo na rekodi ya waliosamehewa na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Kwenye hospitali zote kumewekwa maofisa maendeleo ya jamii ili kukwepa hoja za wakaguzi, kwa sababu tusipofuata hivyo, watu wanaweza wakatumia mwanya huo kusema kuwa, wamesamehe kumbe fedha za umma zimetumika vibaya," alisema.

Dk. Mollel alizielekeza hospitali zote kuhakikisha wagonjwa wa dharura hasa wajawazito wanapokwenda kufuata huduma, wanahudumia kwanza, kisha malipo yafuate baadaye ili kuepusha vifo vinavyozuilika.

Alisema katika huduma ya mama na mtoto, serikali ilipitisha bajeti ya Sh. bilioni 200, lakini mahitaji yake kwa mwaka ni Sh. bilioni 220, kwa hiyo kuna hatua nyingine zinafanywa ili kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kwa uhakika.

Katika swali la msingi, Bonna alihoji hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa madaktari wanaoendelea kuzuia mwili kutokana na deni la matibabu kinyume na maelekezo ya serikali.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel, alisema miili huwa inazuiliwa na uongozi wa hospitali na wala si suala la madaktari.

"Na katika maeneo ambayo tumefanya ufuatiliaji ili kuchukua hatua za kinidhamu kwa viongozi husika, tumebaini ndugu wa marehemu ndio waliokataa kufuata utaratibu uliowekwa ili kuzuia hoja za ukaguzi na ndugu hao wakikimbilia kulalamika kwenye vyombo vya habari na kwa viongozi," alisema.



Koplo Alfred Mtawali wa Kituo cha Polisi Kati Arusha, akitoa elimu ya matumizi ya tiketi mtandao kwa abiria ndani ya basi, katika kituo cha mabasi ya mikoani, jijini humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaojifungua watoto njiti sasa kicheko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeridhia hoja ya kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mwajiriwa ambaye atajifungua mtoto njiti kwa kujumuisha na muda uliobaki kufikia wiki 40 za ujauzito huku baba akipewa siku saba za mapumziko.

Hoja hiyo imekuwa ikipigiwa chapuo kwa muda mrefu na Taasisi ya Doris Mollel, Mtandao Haki ya Afya ya Uzazi, TWPG, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) ili kulinda ustawi na afya za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati ambao wanahitaji muda wa kutosha wa uangalizi wa mama.

Majadiliano kuhusu hoja hiyo yalianza rasmi na wadau hao mwaka 2017 kisha kupelekwa Bungeni mwaka 2018.

Akiwasilisha jana bungeni maelezo ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi namba 13 wa Mwaka 2024, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema awali katika Muswada ilipendekezwa muda wa wiki 36 kama ukomo wa muda wa mtoto kutimia.

Hata hivyo, alisema baada ya majadiliano na kamati, serikali ilikubaliana na mapendekezo ya kuongezwa muda huo hadi kufikia wiki 40 na kuongeza muda wa likizo ya baba ambaye atapata mtoto njiti kuwa siku saba badala ya tatu.

Pia alisema kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha mwajiri kumpatia mwajiriwa likizo bila malipo isiyozidi siku 30 ili kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mwajiriwa kupata likizo bila malipo kutokana na majanga au dharura zinazoweza kujitokeza.

Pamoja na hayo, kifungu cha 14 kinapendekezwa kubainisha aina ya mikataba ya muda maalum ili kuongeza wigo wa mazingira ambayo mtu anaweza kuajiriwa kwa mkataba wa kipindi maalum, ikiwamo mikataba ambayo mwajiriwa anaajiriwa kwa muda ili kuendana na ongezeko la wingi wa kazi, kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo ili kuwajengea uwezo na kufanya kazi nyingine za misimu.

Pia alisema mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuingia katika makubaliano ya namna watakavyofanya kazi katika hali ya dharura inayoweza kuathiri uzalishaji mahali pa kazi wakati wa magonjwa ya milipuko na matukio ya dharura.

Kadhalika, alisema kifungu cha 37 kimeweka masharti yanayozuia mwajiri kutoanzisha au kuendelea na shauri la nidhamu dhidi ya mwajiriwa pale ambapo mgogoro huo upo mbele ya Tume au Mahakama ya Kazi ili kuzuia uingiliaji wa mchakato kushughulikia migogoro.

Katika muswada huo, pia alisema fidia zimeainishwa kulingana na aina ya mgogoro na kuweka ukomo wa chini na wa juu wa fidia inayotolewa kwa mwajiriwa aliyeachishwa kazi isivyo halali huku Kifungu cha 41A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu afua kwa uvunjaji wa mkataba wa ajira ya muda maalumu.

Pia alisema kifungu cha 71 kimeweka masharti ya utaratibu wa kuanza kutumika kwa mikataba ya hali bora inayoingiwa na wakuu wa taasisi za umma. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya sheria hii na utaratibu uliowekwa kwenye sheria zinazosimamia utumishi wa umma.

Hata hivyo, alisema vyama vya wafanyakazi vimewezeshwa kwa pamoja kuingia mikataba ya hali bora na mwajiri au vyama vya waajiri kwa ajili ya kuanzisha majukwaa ya ushiriki wa waajiriwa mahali pa kazi.

Alisema kifungu cha 94 kimeweka masharti ya kuzuia wahusika wa mgogoro kuwasilisha maombi ya mapitio kwa maamuzi madogo ya Tume isipokuwa kama maamuzi hayo yana athari ya kumaliza mgogoro.

Akisoma maoni ya Kamati Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq alishauri serikali kuona namna ya kufanya maboresho katika sheria ili kuruhusu pia wanaojifungua watoto wenye mahitaji maalum kama vile usonji, vichwa vikubwa, mgongo wazi, mdomo sungura, matundu kwenye moyo, seli mundu ili kupewa likizo maalum ya uzazi pindi wanapojifungua.

Naye Mbunge wa Mchinga (CCM), Salma Kikwete aliwataka wanaume watakaopata likizo ya wiki moja baada ya wake zao kujifungua watoto njiti, kutotumia fursa hiyo kwa shughuli nyingine nje ya kuwasaidia wake zao.

AJIRA ZA WAGENI

Mavunde alisema Kifungu cha tisa cha Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436 kimeweka masharti ya kumtaka raia wa kigeni mwenye kibali cha kazi daraja A anayekusudia kujihusisha na kampuni nyingine anayomiliki hisa kupata idhini ya Kamishna wa Kazi badala ya kibali kingine cha kazi.

Alisema marekebisho hayo yanalenga kuondoa usumbufu na kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa mwekezaji ambaye ni raia wa kigeni na baada ya kupata kibali cha kazi kwa kampuni moja hatahitajika kupata kibali kingine kwa kampuni nyingine atakayomiliki hisa.

Alisema kifungu cha 10 kimeweka masharti ya kuzuia urejeshwaji wa ada ya maombi ya kibali cha kazi ili kutoa ufafanuzi kwa waombaji wa vibali vya kazi kuhusiana na ada zinazolipwa wakati wa maombi.

Aidha, kifungu cha 12 kitawawezesha wakimbizi wenye hadhi stahiki kuendelea kufanya kazi bila kubanwa na sharti la ukomo wa muda wa kibali cha kazi.

"Vilevile, kifungu hiki kinarekebishwa ili kuwezesha maombi ya kuhuisha kibali cha kazi kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kazi angalau miezi miwili kabla ya kuisha kwa muda wa kibali," alisema.

## TAKUKURU yabaini upotevu wa mapato stendi ya Msamvu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa imebaini kuwapo kwa mianya ya upotevu mkubwa wa mapato wakati wa kutoa huduma katika Stendi Kuu ya Msamvu ya Mabasi yaendayo Mikoani.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa humo, Christopher Mwakajinga, aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, 2024.

Mwakajinga alisema mianya ya upotevu wa mapato iliyobainika ni wakusanyaji mapato kutotoa stakabadhi kwa baadhi ya abiria au kutoa zilizotumika.

"Mianya mingine ni kutotoa stakabadhi kwa madai ya kukosekana kwa chenji, wakusanya ushuru kupewa rola chache za stakabadhi zisizoendana na makisio ya makusanyo kwa siku husika," alisema.

Mwakajinga alisema baada ya kupata taarifa ya kuwapo kwa miaya hiyo walifanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato katika Stendi ya Msamvu kwa siku tatu mfululizo kilichoanzia Desemba 24, mwaka jana kwa saa 24.

Alisema katika kipindi hicho mapato yaliyokusanywa yalikuwa ni Sh. milioni 18.083, ambapo Desemba 12, mwaka jana zilipatikana Sh. milioni 5.6 siku iliyofuata (Desemba 13), Sh. milioni 6.4 na siku ya mwisho (Desemba 14) kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni Sh. milioni 5.9.

"Katika tathmini iliyofanyika kwenye ukusanyaji wa mapato kwa mwezi Desemba, mwaka jana, inaonesha makusanyo yaliyopatikana katika siku hizo tatu ndiyo yalikuwa mapato ya juu zaidi kukusanywa kwa mwezi husika," alisema Mwakajinga.

Alisema ufuatiliaji huo ulibaini kuwapo kwa mianya ya upotevu wa mapato kwa huduma zinazotolewa katika stendi kuu na kwamba, mianya hiyo isipozibwa mapato yatazidi kupotea kwa kuishia mikononi mwa wajanja wachache.

Alisema TAKUKURU Mkoa imeamua kuwa mchakato wa ufuatiliaji mapato katika vyanzo vyote vya ndani ikiwamo kwenye stendi hiyo kuwa endelevu.

Alisema kwa kushirikiana na Manispaa ya Morogoro inafanyia kazi yale yote yaliyobainika katika mchakato husika ili kuweza kuwabaini wahusika wote waliomo katika mnyororo mzima wa ufujaji wa mapato katika stendi hiyo ili kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Nitoe angalizo kwa halmashauri zote ndani ya Mkoa wa Morogoro kuhakikisha wanasimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato kama inavyopaswa," alisema Mwakajinga.

Kiongozi huyo aliwakumbusha wananchi wote wanaotumia Stendi ya Msamvu kudai stakabadhi kulingana na huduma wanazopewa.

Mmoja wa wadau wa stendi hiyo ya Msamvu ambaye ni mmiliki wa mabasi yaendayo mikoani, Salum Tembo, alitaka TAKUKURU kuwachukulia hatua kali zikiwamo kuwafikisha kwenye vyombo vya kisheria wahusika wote waliobainika kuwapo kwa upotevu huo wa fedha za

# Wafariki dunia madai kunywa pombe kali

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKAZI watatu wa kijiji cha Bashnet, Babati mkoani Manyara, wamefariki dunia kwa madai ya kunywa pombe kali ambazo bado hazijulikani zinakozalishwa huku Jeshi la Polisi likizuia kuzikwa kwa watu hao mpaka uchunguzi ukamilike.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara Ahmed Makarani, jana alikiri kutokea vifo vya watu hao.

"Tunayo hiyo taarifa tunaendelea na upelelezi hatua za msingi tumeshazifanya sisi hatutazami wapi zinazalishwa bali tunatazama chanzo cha kifo ndiyo tunatafuta chanzo," alisema Makarani.

Aidha, alisema wanasubiri taarifa ya uchunguzi wa daktari kama ni sumu au alikunywa bila kula.

"Ndiyo maana tunafanya uchunguzi wa kina ambapo atafanya daktari na mkemia mkuu wa serikali na wanaweza kutoa mapafu ili wajiridhishe kama ni pombe au sumu," alisema.

Makarani alisema hawawezi kuruhusu kufanyika maziko mpaka wafanye uchunguzi wa kina.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Wilaya ya Babati kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Bashnet, Martin Akonay, akizungumzia suala hilo alikiri kutokea kwa vifo vya watu hao. Alisema wote watatu vifo vimefanana.

Akonay alisema historia ya marehemu hao ni wanywaji sana wa pombe huku akidai mmoja alikufa saa 10:00 Alfajili, wa pili saa 3:00 asubuhi na wa tatu saa 9:00 alasiri.

Mwenyekiti huyo alisema wanasubiri matokeo ya uchunguzi utakaofanywa na daktari na mkemia mkuu ili taratibu za mazishi ndio ziweze kuendelea.

Mmoja wa ndugu wa marehemu ambaye hakuwa tayari kuandikwa majina yake aliiambia Nipashe kuwa walikuwa watano hivyo walikimbizwa hospitali na wawili waliokolewa kwa kutolewa sumu mwilini.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Stephen Wasira, akihutubia katika mkutano wa hadhara wakati wa kumkaribisha, mjini Bunda, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Migogoro 9,000 yaibuliwa Kampeni Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, imesaidia kuibua migogoro na changamoto za kisheria 9,069 tangu izinduliwe rasmi mwaka 2023.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, alipomwakilisha Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko, katika uzinduzi wa kampeni hiyo ya Msaada wa Kisheria mkoani humo ikiwa ni mwendelezo wa programu ya siku tisa ya kutoa huduma hiyo inayofanyika kwa awamu nyingine katika mikoa sita tangu Januari 24, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Shigela, tangu kuanza kwa kampeni hiyo, watu 779,191 wamefikiwa, kati ya hao 300,096 ni wanaume na wanawake ni 300,089.

"Tunaipongeza kampeni hii kwa kuwafikia na kugusa watu wote hawa na kutatua changamoto na migogoro yao mbalimbali kwa njia ya kisheria, hili ni jambo jema sana na tunaamini watu wengi zaidi wenye shida wataendelea kuguswa, ni vema wananchi mnaposikia kampeni hii imewafikia katika maeneo yenu msiache kuitumia hii fursa kwa sababu kwanza ni bure, lakini hata kama una changamoto na unashindwa kujua ni namna gani utapata wanasheria wa kukutatulia hilo jambo lako bado utasaidiwa," alisema Shigela.

Alitaja migogoro iliyotatuliwa na kupata suluhisho la kudumu kuwa ni zaidi ya 1,505 na wanaamini kwamba lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha migogoro mingi inatatuliwa na kupatiwa suluhisho la kudumu.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju, alisema serikali imelenga kupeleka fedha za uwezeshwaji wananchi kiuchumi pamoja na wafanyabiashara na kiasi cha Sh. bilioni 10.5 kimetegwa kwa ajili ya kuwakwamua wananchi kiuchumi na hilo litasaidia kupunguza migogoro iliyopo kwenye jamii.

"Mambo mengine ya ukatili vipigo vya kinamama ni kwa sababu watu hawajawezeshwa kiuchumi, kwa hiyo serikali ya awamu ya sita imelenga kupeleka fedha na uwezeshaji wananchi mpaka ngazi ya chini na kati ya maeneo tunayosimamia ni suala la upatikanaji wa mikopo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo," alisema Mpanju.

Kampeni hiyo ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inaratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria na miongoni mwa huduma za kisheria inazozitoa ni pamoja na eneo la mirathi, migogoro ya ardhi, ukatili wa kijinsia, ndoa na awamu hii inaendelea kwa siku tisa katika mikoa ya Kigoma, Geita, Kilimanjaro, Tabora,Katavi na Mtwara.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji kuona burudani, ufundi lala salama Ligi Kuu

**LIGI** Kuu Tanzania Bara inatarajia kurejea tena leo baada ya kusimama kwa muda kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, michezo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Awali mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara au hatua ya lala salama ilipangwa kurejea tena kuanzia Machi Mosi mwaka huu, ili kupisha kufanyika kwa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Hata hivyo, Shirikisho la Mpira wa Miguu la Afrika (CAF), lilitangaza kusogeza mbele michuano hiyo hadi Agosti 2, mwaka huu na kupelekea Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), kurudisha nyuma kalenda yake.

Bodi ya Ligi tayari imeshatoa ratiba mpya ambayo inaonyesha inaanza na mechi za viporo, leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam mabingwa watetezi wa ligi hiyo wakiwakaribisha Kagera Sugar kutoka Bukoba mkoani Kagera na kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora wenyeji Tabora United watakaribisha Simba.

Mbali na mashabiki na wadau wa soka 'ku-miss vibe' la Ligi Kuu Tanzania Bara, mechi hizo za viporo zinaonekana kama vile ndio za ufunguzi wa msimu kutokana na rekodi ambazo timu zinazokutana zimeweka.

Yanga imekuwa ikipata wakati mgumu ikikutana na Kagera Sugar hapa Dar es Salaam tofauti na wanapocheza ugenini huku Simba akisubiriwa kujibu 'kitendawili' cha kuizuia Tabora United kuvuna pointi kama ilivyofanya kwa mabingwa watetezi na Azam FC.

Mambo haya mawili yanaongeza mvuto wa kusubiriwa kwa michezo hiyo, lakini pia kukata kiu ya mashabiki na wadau wa soka ambao waliikosa burudani ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Wakati kila timu itaanza mzunguko wa pili, ingawa baadhi yao wameshacheza mechi 16, ikiwa na malengo yake, tayari baadhi zimeshajipambanua zina malengo yapi katika msimu huu unaoendelea wa mwaka 2024/2025.

Mpaka sasa kuna makundi matatu, kundi la kwanza ni zile ambazo zinaendelea kupambana kuwania taji na zinaonyesha wazi zina kiu kubwa ya kutwaa ubingwa kwa kila siku kujiimarisha na kujipanga kuvuna pointi tatu kwa sababu inaamini bado taji liko wazi.

Kundi lingine ni zile timu ambazo zimeshajidhihirisha zinahitaji pointi muhimu ili kujiweka mahali salama katika msimamo lakini pia zikihitaji kumaliza kwenye nafasi nne za juu na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na CAF ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini pia kuna kundi ambao lenyewe malengo yake sasa ni kuvuna pointi na kujinusuru na janga la kushuka daraja kwa sababu kwao itakuwa ni miujiza zikibeba taji hilo, kutokana na kutokuwa na matokeo chanya katika mechi za mzunguko wa kwanza.

Hawa ndio hucheza kwa kukamia na wakati mwingine mechi zao hupoteza mvuto.


Katika soka lolote hutokea hasa pale michezo iliyobaki ni mingi, huu ni wakati wa viongozi, makocha na wachezaji kuongeza utulivu na hatimaye kusaka ushindi na kudhihirisha matokeo ya mzunguko wa kwanza yalitokana na 'kuteleza'.

Pia wachezaji kuonyesha kandanda safi sio tu kutaisaidia kupata matokeo chanya timu yao, ubora huo utawaongezea thamani wachezaji na kujiweka 'sokoni' kuelekea maandalizi ya msimu mpya.

Wachezaji kuonyesha nidhamu ndani na nje ya uwanja itawasaidia kuwaongezea mashabiki kujitokeza kwa wingi viwanjani kwa sababu wataamini wanakwenda kushuhudia vipaji na si vurugu au faulo ambazo hazistahili kutokea kwa wanamichezo.

Tunawakumbusha tunatarajia kushuhudia burudani na ufundi katika hatua ya mzunguko wa pili au lala salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Mashabiki msiogope kuhofia timu AFCON, zama zimepitwa

**KATIKA** Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika kuanzia Desemba 21, mwaka huu huko Morocco, Tanzania (Taifa Stars), imepangwa katika Kundi C ikiwa pamoja na Nigeria, Uganda na Tunisia.

Baada ya droo hiyo kufanyika, kumezuka mijadala mbalimbali kutoka kwa baadhi ya wadau na mashabiki wa soka juu ya ugumu wa kundi ambalo Taifa Stars iko.

Wengi hawasemi ni kundi la kifo, ila ni kundi gumu ambalo hawana uhakika kama Stars inaweza kutoboa na kusonga mbele hatua inayofuata.

Sababu kubwa ni timu wapinzani ambao wamepangwa kundi moja.

Nigeria ni moja kati ya majina makubwa si barani Afrika tu, bali dunia nzima linapokuja suala la mpira wa miguu.

Tunisia nayo ni hivyo hivyo, ni moja kati ya timu kubwa ya 'kutisha' linapokuja suala la soka Afrika na duniani pia.

Uganda siyo timu ngumu au yenye jina sana kwenye soka Afrika, lakini ni moja kati ya timu inayoipa ugumu na changamoto kubwa Tanzania zinapokutana, iwe katika timu za wakubwa, wanawake mpaka kwa vijana wa umri wote.

Kwa sasa mpinzani mkubwa wa soka la Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) kwa Tanzania ni Uganda.

Na hata matokeo yake huku hayajulikani yatakuwaje zinapocheza.

Oktoba tu mwaka jana, timu za Tanzania na Uganda zilikutana katika mechi za kuwania tiketi ya kufuzu fainali za Afrika chini ya miaka 20. Katika mchezo wa nusu fainali, lakini kwenye mechi ya AFCON chini ya miaka 17 iliyochezwa hapa nchini, Uganda ilishinda mabao 2-1 katika mchezo wa fainali. Hii inaonyesha upinzani uliopo.

Hakuna anayepinga Kundi C ni gumu, lakini kinachotakiwa ni kujipanga na si kuogopa.

Kwa miaka ya hivi karibuni tumeanza kuona baadhi ya nchi ambazo zamani zilikuwa chini kisoka na zilikuwa zikipigwa mabao mengi, zikianza kuwa tishio kwa yale mataifa makubwa ambayo yalionekana hatari.

Mfano timu kama Cape Verde, Comoro, Equatorial Guinea, Botswana, hazikuwa juu kisoka na hata zinapopangwa na timu iwe klabu au timu za taifa, moja kwa moja timu zingine zinaona zimepata mchekea, lakini siyo sasa.

Kwa sasa ukipangwa nazo jiandae kisawaswa, si tena wale wa miaka ile ambao walitambulika kama vibonde.

Hapa ukiondoa Cape Verde tu ambayo haijafuzu AFCON, zote ninazokutajia zimefuzu, kitu ambacho ilikuwa nadra sana kukikuta miaka ya 1970, 1980, 1990, hadi miaka ya 2000.

Hivi ninavyoandika, Comoro iko Kundi A, huyu huyu kibonde wa miaka ya 1980 hadi 1990.

Ilikuwa ni ajabu kukuta timu hiyo ikishinda hata mchezo mmoja tu. Equatorial Guinea ipo Kundi E, Botswana nayo imetupwa Kundi D.

Na tusishangae katika AFCON 2025, nchi hizo, timu zisizotegemewa ndiyo zinaweza kushangaza wengi na kufuzu hatua inazofuata.

Soka kwa sasa dunia limebadilika kabisa, ni kujipanga, mfumo, mbinu na nidhamu ya wachezaji ndivyo vinavyoamua uwanjani timu gani ishinde.

Zile zama za kutegemea vipaji vya machezaji mmoja mmoja kuamua mechi kama kina Nwanko Kanu, Austin Jay Jay Okocha, Maradona, Pele, zimepitwa na wakati na inaonekana kwa sasa aina ile ya wachezaji kama haipo basi imepungua sana.

Watanzania tusitishwe na majina ya nchi kubwa za mpira kwa wakati huo. Kwa sasa soka la nchi hii limepiga hatua sana na wala si ajabu Stars ikavuka kwenda raundi ya pili.

Kinachotakiwa ni kufanyika kwa uteuzi mzuri wa wachezaji ambao wana viwango bora kwa wakati husika, pamoja na maandalizi ya kina. Hakuna kinachoshindikana kuondoka na mmoja kwenda hatua inayofuata au kufika robo fainali, haidhuru kuwaacha wote wawili tukaondoka na Uganda.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

## HABARI KITAIFA

# Waziri asifu udhibiti hujuma mazao ghalani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, ameipongeza Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa kuweka mfumo wa kamera kwenye maghala ambao utasaidia kubaini wanaohujuma mazao na kuisababishia hasara serikali na wakulima.

Jafo alitoa pongezi hizo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala baada ya kuzindua mfumo wa kutumia kamera za kidijitali na stika ya utambuzi wa ghala ikiwamo logo kwa ajili ya kutambua maghala.

Alisema mfumo huo wa kuweka kamera pamoja na kusaidia usalama kwenye maghala pia utawezesha kutambuana na kurahisisha shughuli za usimamizi nchini kote tofauti na ilivyokuwa awali.

Mfumo wa stakabadhi ghalani, alisema utafanikisha kuwa na usimamizi mzuri kutokana na kupanda bei kwa mazao kwa hivi sasa, tofauti na huku nyuma ambako bei ilikuwa imeshuka na kukatisha tamaa wakulima.

"Hata hivyo napenda kuwapongeza bodi hii kuwa na mfumo wa kamera, utaweza kubaini maeneo wanayohujumiwa ya maghala yetu ya mazao, hivyo nichukuwe nafasi hii kuwapongeza kwa hatua hiyo ambayo maghala hayo hivi sasa kuna kamera," alisema.

Katika hatua nyingi aliwataka watumishi wa bodi hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii kwenye utendaji wao na waache kupoteza muda kwa kuwa wanatakiwa kuonyesha thamani yao katika utendaji wao.

"Tengenezeni umoja utakaoleta mafanikio ndani ya bodi hiyo na taassisi zingine mnazofanya kazi badala ya kukwamisha maendeleo yanayotakiwa," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Asangye Bangu, alisema kuwapo kwa mfumo huo wa kutumia kamera na uwepo wa logo kutasaidia kuongeza tija katika usimamizi wa maghala nchini.

# THBUB yatoa mapendekezo kukomesha mauaji ya raia

**Na Romana Mallya**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imelaani mauaji ya Jumanne Juma (28), mkazi wa Mtaa wa Kimara B, Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, anayedaiwa kuchomwa na mafuta ya petroli na watu aliokuwa akiwafanyia kazi za nyumbani, kwa madai ya kuwaibia Sh. 200,000.

Kutokana na tukio hilo, tume hiyo imetoa mapendekezo matano kwa Jeshi la Polisi, serikali za mitaa, viongozi wa dini, wananchi na asasi za kiraia ili kuyakomesha.

Mwenyekiti wa THBUB, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, alisema juzi kwamba, taarifa za Jeshi la Polisi zinaeleza kuwa watu waliomuua Jumanne walimfuata nyumbani kwake majira ya saa 4 usiku kumtaka waondoke naye wakamlipe malipo yake pamoja na kumpatia kazi nyingine.

"Hata hivyo, baada ya kuondoka naye walimpeleka mahali, wakanunua mafuta ya petroli na kumchoma moto.

"Katika ufuatiliaji wake, THBUB imebaini baadhi ya wananchi bado hawaiheshimu Katiba ya nchi kama inavyoelekeza katika Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na sheria za nchi na hivyo, kujichukulia sheria mikononi," ilisema taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Aidha, Jaji Mstaafu Mwaimu alisema vitendo vya mauaji vilivyotokea hivi karibuni vimeambatana na ukatili dhidi ya ubinadamu na kuna viashiria vya wananchi kutokuwa na imani na vyombo vya usimamizi wa haki.

Alisema kutokana na tukio hilo ambalo limesababisha kifo cha Juma, THBUB inapenda kutamka kuwa kitendo hicho ni ukiukwaji wa haki ya kuishi kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 14 Katiba ya mwaka 1977.

"Hivyo, THBUB inalaani vikali vitendo hivyo; na ukatili dhidi ya binadamu ambao ni kinyume na Ibara ya 13(6)(e) ya Katiba. THBUB inatambua jitihada za zilizofanywa na Jeshi la Polisi kwa kuwakamata watuhumiwa," alisema.

Jaji Mstaafu Mwaimu alisema pamoja na hayo, THBUB inatoa mapendekezo kwa Jeshi la Polisi kuendelea kuchukua hatua mahsusi kuimarisha ulinzi katika maeneo ya wananchi kuwezesha kupata taarifa za mapema.

Alisema kupata taarifa mapema ma kuhusu kuwapo viashiria vya uvunjifu wa sheria, ikiwa ni pamoja na mauaji na vitendo vya ukatili.

"Liimarishe ulinzi shirikishi kupitia vituo vya Polisi Kata kwa kuongeza idadi ya vituo na idadi ya askari ili kuongeza ufanisi.

"Kwa upande wa mamlaka za serikali za mitaa katika ngazi zote tunapendekeza ziwe na mipango madhubuti ya kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo yao," alisema. Mapendekezo mengine, aliyataja ni viongozi wa dini kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu ya dini na maadili na kukemea uovu unaotokea nchini.

Kadhalika, alisema wananchi kujenga utamaduni wa kuheshimu sheria za nchi, haki za binadamu, kufuata namna bora ya kupata suluhu ya migogoro na kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi.

"Washirikiane na vyombo vya dola kufichua maovu kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili kuzuia matukio kama hayokutokea.

"Asasi za kiraia na vyombo vya habari kuendelea kutoa taarifa za matukio ya uhalifu kwa wakati na kushiriki kwa ukamilifu katika kutoa elimu kwa umma kuhusu taratibu zilizoko za namna ya kushughulikia masuala mbalimbali ya kijamii kupitia sheria na hivyo, kulinda haki za binadamu na utu wa mtu," alisema.

Aidha, Jaji Mwaimu alisema THBUB inatoa pole kwa ndugu, jamaa na wanafamilia waliopoteza mpendwa wao katika tukio hilo na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano katika jitihada za kukomesha na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora.




Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. bilioni 13 kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Umoja wa Wakulima wa zao la Tumbaku nchini (TCJE), John Ntelizyo (kushoto), jijini Dodoma juzi, kwa ajili ya kusaidia wakulima wa zao hilo nchini. Kulia ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mpango kituo forodha Kabanga kufanya kazi saa 24

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema inafanya jitihada ili Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) Kabanga, kinachotoa huduma kati ya Tanzania na Burundi, kufanya kazi kwa saa 24 ili kuongeza ufanisi.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema hayo juzi alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoho, aliyetaka kujua mkakati wa serikali wa kuwezesha vituo vya forodha vya Murusagamba na Kabanga, kufanya kazi kwa saa 24.

Chande alisema kuwa Kituo cha Forodha cha Kabanga ni Kituo cha Pamoja (OSBP) cha kutoa huduma za forodha kati ya Tanzania na Burundi kina miundombinu wezeshi kama vile taa za ulinzi, vyombo vya ulinzi na usalama, na maeneo ya kukagulia bidhaa, wasafiri na wafanyakazi, hivyo kuwa na uwezo wa kufanya kazi saa 24 kwa upande wa Tanzania. "Ili kituo hicho kitoe huduma saa 24, upande wa Kobero nchini Burundi unapaswa pia kuwa tayari kutoa huduma hizo saa 24", alisema.

Chande alisema kwa sasa Kituo cha OSBP Kobero kwa upande wa Burundi kinatoa huduma kwa saa 12 tu, hivyo jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kuwezesha mazingira ya kituo hicho kufanya kazi saa 24, hususan ulinzi na usalama.

Kuhusu kituo cha Murusagamba, Chande alisema hicho ni kidogo cha forodha kinachofanya kazi ya uzuiaji na hufanya kazi ya kuzuia magendo kwenye maeneo ambayo mwenendo wa bidhaa na watu ni mdogo.

Naibu Waziri Chande alisema kutokana na udogo wa mwenendo wa bidhaa na watu katika kituo cha Murusagamba, uwezekano wa kituo hiki kufanya kazi saa 24 kwa sasa haupo.

Akijibu maswali ya nyongeza kuhusu ufungaji wa kifaa cha ukaguzi eneo la Mutukula lililoko mpaka wa Tanzania na Uganda na Kituo cha Horohoro, Tanga kati ya Tanzania na Kenya, Chande alisema kwa upande wa Mutukula tayari mkandarasi yuko eneo la mradi kwa ajili ya kufunga kifaa hicho na upande wa Horohoro, serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inaangalia utekelezaji wake.

Pia alisema mazungumzo yanaendelea kuhusu uwezekano wa Kituo cha Forodha cha Malindi, Zanzibar kufanya kazi saa 24 kwa kuwa kwa sasa kinahudumia makontena 2,000 kwa mwezi licha ya kufanya kazi kwa saa 12.

Alisema serikali inaendelea na mazungumzo na upande wa Zanzibar na kwamba kukamilika kwa mazungumzo hayo kutawezesha huduma hiyo.

# ‘Fichueni wakopeshaji wa mikopo umiza’

**Na Asia Singano,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI na wananchi wa Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, wametakiwa kutoa taarifa kwa maofisa maendeleo ya jamii wa kata zao kuhusu wakopeshaji wasio rasmi wanaokopesha kinyume cha taratibu na Sheria za Huduma Ndogo za Fedha ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Wito huo ulitolewa juzi na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Dk. George Kasibante, alipotembelewa na kufanya mazungumzo na timu ya wataalamu wa kutoa elimu ya fedha, kutoka Wizara ya Fedha na taasisi zake kabla ya timu hiyo kwenda katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo kutoa elimu ya fedha kwa wananchi.

Alisema utoaji taarifa kuhusu uwapo wa watoa huduma za fedha wasio waaminifu utasaidia serikali kuwatambua na kuwachukulia hatua za kisheria na kuwafanya kufuata Sheria za Huduma Ndogo za Fedha ikiwamo kusajiliwa rasmi na kuleta unafuu wa kukopa kwa wananchi na kukuza kipato chao.

‘’Naamini hawa watu tunaishi nao majumbani. Wengine ni wakopeshaji ambao baadhi hawatambuliki kwa hiyo wito wangu kwa wananchi wakibaini kuna watu wa namna hiyo, basi watoe taarifa kwenye ofisi za kata zao,’’ alisema.

Dk. Kasibante aliipongeza Wizara ya Fedha kwa kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma kwa kuwa mafunzo hayo yanawafanya wananchi kupata uelewa juu ya matumizi sahihi ya fedha, masuala ya mikopo na kuwakwamua kiuchumi huku akishauri suala hilo kuwa endelevu.

Akitoa elimu ya fedha kwa wananchi wa Monduli, Ofisa Usimamizi wa Fedha, Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Salim Kimaro, aliwasisitiza wahamasishaji wa vikundi vya huduma ndogo za fedha kujisajili na kushiriki mafunzo mbalimbali yanayotolewa ili kuwa wabobezi kuhusu masuala ya fedha huku akiwaasa wajasiriamali kuhakiki usajili wa wahamasishaji wa vikundi vyao.

‘’Waulizeni wale wahamasishaji mnaowaita walimu wa vikundi mwenzetu umesajiliwa tunaomba tuone cheti chako kwa sababu mkiwa na wahamasishaji ambao hawana elimu ya uhamasishaji wa masuala ya fedha ataelekeza kinyume na taratibu,’’ alisema Kimaro.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Fedha inaendelea kutekeleza programu ya kutoa elimu ya fedha kwa umma ili kuhakikisha wananchi wote wanapata uelewa juu ya matumizi sahihi ya fedha.

‘’Hii ni awamu ya tatu ya Programu ya Elimu ya Fedha, tayari tulishatembelea na kutoa elimu ya fedha katika mikoa kumi na mbili, huu mkoa wa Arusha ni wa kumi na tatu.

Baadhi ya wajasiriamali waliohudhuria mafunzo hayo ya elimu ya fedha walisema mafunzo hayo yatawasaidia katika shughuli zao za ujasiriamali huku wakiomba mafunzo hayo yawe endelevu.



Mkurugenzi wa Taasisi inayojishughulisha na afya bora ya akili ya Falimy Vibes Foundation, Dk. Mayrose Majinge, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa Tuzo za Wazalendo za Watu Mashuhuri, unaotarajiwa kufanyika Februari 13, mwaka huu. Kushoto ni mwanachama wa taasisi hiyo, Henry Majinge. **PICHA: JUMANNE**

# Wapewa angalizo kilimo msimu wa masika

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAMU wa kilimo na mabadiliko ya tabianchi wametoa angalizo kwa wakulima kuomba ushauri kwa maofisa ugani mazao ya kulima msimu wa mvua za masika, kutokana na utabiri kuonesha zitanyesha chini ya wastani.

Wamesema kutokana na utabiri uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuonesha mvua hizo zitanyesha chini ya wastani, ni muhimu kuchukua hatua hizo kwa kuomba ushauri kwa wataalamu badala ya kulima na kupata hasara.

Januari 23, mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang’aa, akizungumza na waandishi wa habari, alisema mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni, baadhi ya kanda zitanyesha chini ya wastani na juu ya wastani.

Baadhi ya maeneo ambayo yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani aliyataja ni ya Pwani ya Kaskazini, Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma na Ukanda wa Ziwa Victoria ikiwamo mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga na magharibi mwa mikoa ya Simiyu na Mara.

Alisema mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kaskazini-Mashariki pamoja na Mashariki mwa mikoa ya Mara na Simiyu, huku zile za wastani hadi chini ya wastani zikitarajiwa katika maeneo ya Pwani ya Kaskazini, Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma na Ukanda wa Ziwa Victoria.

Kutokana na utabiri huo, Nipashe ilipowatafuta wataalamu wa kilimo ili kutoa ushauri bora wa wakulima akiwamo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Dk. Elly Ligate, aliwashauri kujiandaa vizuri na kufuatia taarifa hiyo kwa ukaribu.

Alisema wakulima wanapaswa kuomba ushauri kutoka kwa maofisa ugani wa maeneo yao kuhusu mazao wanayopaswa kulima, ili kuepuka hasara zinazoweza kusababishwa na mvua kunyesha chini ya wastani.

Alisema endapo mkulima ataona kuna haja ya kulima zao alilozoea kama vile mahindi, anashauriwa kuchagua mbegu zinazokomaa kwa muda mfupi ili kuepuka zisikae shambani muda mrefu na kuathiriwa na ukame.

Kadhalika, ameshauri wanapotafuta mbegu, wachague zile ambazo zinastahimili magonjwa kwa sababu ukame unaambatana na wadudu wanaoshambulia mimea na kusababisha magonjwa.

“Kukiwa na ukame tu, wadudu huwa wanashambulia mimea na magonjwa yanalipuka, kwa sababu mmea unakuwa hauna nguvu ya ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu,” alifafanua.

Dk. Ligate, aliitaka serikali kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ili kuwasaidia wakulima kulima bila kujali kuna mvua au la, hali itakayoihakikishia nchi usalama wa chakula.

Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Dk. Primitive Mboyerwa, alisisitiza wakulima kupanda mazao yanayohimili mvua kidogo kama vile mtama na mihogo pamoja na yale yanayokomaa kwa muda mfupi.

Kadhalika aliwataka watumie mbegu bora zilizodhibitishwa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI) pamoja na matumizi sahihi ya mbolea.

Kadhalika alishauri wakulima kupima afya ya udongo kabla ya hawajapanda mazao maana itawasaidia kujua rutuba ya udongo.

“Hii pia itawasaidia kujua mbolea ipi itumike ili kuweza kupata mavuno mengi. Watizame aina ya mazao yanayostahili kupandwa kwenye mashamba yao,” alisema.

Dk. Mboyerwa aliwashauri wakulima wanaolima mazao yasiyostahimili ukame kama vile mahindi kuweka matandao kwenye mashamba yao ili yatunze unyevu au kuchimba mashimo marefu ambayo yatahifadhi maji mvua zinaponyesha, ili yatumike kustawisha mashamba kipindi cha ukame.

“Kwa upande wa mifugo, wajitahidi kutumia na kuhifadhi vizuri chakula cha mifugo, ili kitumike kwa muda mrefu,” alisema.

Kadhalika aliishauri serikali kuhimiza maofisa ugani wafikishe taarifa za utabiri wa hali ya hewa kwa wakulima, ili wachukue tahadhari na kujiandaa vizuri na matokeo yoyote yatakayoletwa na mvua.

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Pius Yanda, alishauri wakulima kutumia mbegu za muda mfupi ambazo zinastahimili ukame ili kuepuka hasara zinazoweza kusababishwa na mvua kunyesha chini ya wastani.

“Ninashauri pia, kuanzishwa utaratibu wa kujenga miundombinu ya kuvuna na kuyahifadhi maji mvua ili yatumike katika kilimo cha bustani na matumizi ya nyumbani kwenye maeneo yenye ukame.

“Mvua zinaweza kunyesha cha muda mfupi, lakini zikanyesha nyingi na kusababisha mafuriko, kwa hiyo yale maji yanatakiwa yavunwe ili yasaidie katika umwagiliaji mazao,” alisema.

Mkulima wa mahindi kutoka Kijiji cha Mkindo, Wilaya ya Mvomero, mkoani Morogoro, Issa Jumanne, alisema anategemea mvua hizo kwa ajili ya kilimo, hivyo kama zikinyesha chini ya wastani, anahofu kupata hasara kwa sababu hafahamu njia mbadala ya kuiepuka.

“Sisi wakulima wa hali ya chini sasa hivi tunalima kwa kubahatisha, Mungu akitusaidia akaleta mvua ya wastani basi tunapata mazao mazuri, ikinyesha chini ya kiwango au juu ya kiwango tunapata hasara, tunasubiri tena msimu mwingine,” alisema.

Issa alitaka serikali kupitia kwa maofisa ugani kuitisha vikao na wakulima na kuwapa elimu kuhusu matarajio ya mvua katika msimu husika na namna wanavyoweza kufanya kuepuka hasara.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Mtakwimu, Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2022/23, asilimia 21.6 ya mashamba makubwa yaliyolimwa katika msimu wa mvua za vuli yaliathiriwa kikamilifu na majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya hali ya hewa ikiwamo ukame, huku asilimia 9.2 yaliathiriwa kwa kiasi.

Katika mvua za masika, asilimia 9.7 ya eneo lote lililopandwa na mashamba makubwa liliathiriwa kikamilifu, huku asilimia 13.2 likiathiriwa kwa kiasi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mazao makuu yaliyolimwa katika mwaka huo ni mahindi, mpunga na mtama.

Kwa upande wa Tanzania Bara, mahindi ndiyo yaliyokuwa na uzalishaji mkubwa zaidi kwa tani 6,970,859, huku Zanzibar mpunga ukiongoza kwa uzalishaji kwa tani 9,485.

Taarifa hiyo pia, ilishauri kuimarisha mifumo ya tahadhari ya mapema kwa ajili ya utoaji wa taarifa za tahadhari kwa wakati kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa.

Mbinu mbadala za usimamizi wa majanga na kupunguza athari zake katika kilimo zinapaswa kuboreshwa.





# RAS asisitiza mahakama tembezi kufikia wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida Dk.Fatuma Mganga, ameishauri mahakama kutumia mahakama tembezi kuwafikia wananchi wa vijijini ambao wanashindwa kufika mijini kupata msaada wa kisheria kutokana na shida mbalimbali zinazowakabili.

Akizungumza juzi wakati wa Wiki ya Sheria, aliwataka viongozi wa mahakama ya Singida kufika vijijini kwani wananchi wengi wa matatizo mengi na wamekuwa wakikosa haki zao za msingi za kuhudumiwa.

"Vijijini hakuna mahakama za mwanzo wala za wilaya kwa hiyo niwashauri na niwaombe zile 'mobile courts' ambazo zimeanzishwa sasa ni wakati wake twendeni kule vijijini na vitongoji kusikiliza matatizo kuwapunguzia adha zinazowakabili," alisema.

Naye Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Singida, Allu Nzowa, alisema taasisi za haki jinai zina mchango mkubwa katika kulinda amani na utulivu, kukuza utawala wa sheria, kukuza uchumi na biashara ya uwekezaji.

Alisema taasisi hizo pia zina nafasi ya kujadili na kutathmini mambo yanayoathiri utendaji wao na kuandaa mapendekezo yenye tija yatakayoleta ufanisi na kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini.

Naye Mkurugenzi wa Shirika linatoa huduma za msaada wa sheria kwa jamii Singida, Teddy Mande, alisema wananchi wengi wanapoteza haki zao kutokana na kutofahamu ni wakifanye kutetea haki zao.

Alisema kutokana na hali hiyo ni wakati sasa kwa taasisi na mashirika yasio ya kiserikali ambayo yanahusisha na utoaji msaada wa kisheria kuongeza kasi ili wananchi waweze kupata haki zao.

# Elimu yatiliwa mkazo tatizo afya ya akili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Lawala, amesema hivi sasa nguvu kubwa imeelekezwa katika utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu tatizo la afya ya akili badala ya kusubiri wagonjwa.

Dk. Lawala alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya utiaji saini hati ya makubaliano kati ya hospitali hiyo na Taasisi ya Vanessa Amada. Hati hiyo ya makubaliano inalenga kuimarisha jitihada za pamoja katika kuhakikisha huduma bora za afya ya akili zinapatikana kwa vijana na watoto.

Aidha, Dk. Lawala alisema katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, hospitali hiyo imeamua kuwekeza nguvu zaidi kwenye kutoa elimu badala ya kusubiri wagonjwa.

"Tumeona ni muhimu kuzungumza na jamii yenye afya kuhusu tatizo la afya ya akili badala ya kuwekeza nguvu kwenye ugonjwa kwani imekuwa ni vigumu sana kuwapata watu kutokana na namna ilivyo katika jamii zetu.

"Jamii zetu bado kwanza hazina uelewa lakini pia tatizo jingine ni unyanyapaa hivyo kama elimu itafika kwa jamii na kupata uelewa wa kutosha kuhusu tatizo hili tutaongea lugha moja tofauti na ilivyo sasa," alisema Dk. Lawala.

> **"Tumeona ni muhimu kuzungumza na jamii yenye afya kuhusu tatizo la afya ya akili badala ya kuwekeza nguvu kwenye ugonjwa kwani imekuwa ni vigumu sana kuwapata watu...**

Alisema kama jamii itapata uelewa wa kutosha kuhusu tatizo la afya ya akili, hatua hiyo itasaidia watu kujitokeza mapema kupata huduma katika hospitali hiyo.

"Hivi sasa watu hawajitokezi kutokana na kukosa elimu wapi waende kupata huduma ama unyanyapaa ambao bado upo katika jamii yetu kuhusu tatizo hili," alisema.

Naye Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Vanessa Amada, alisema ushirikiano huo unaongeza chachu ya mabadiliko na nguvu ya kufanya kazi zaidi katika kuleta athari chanya kwa jamii.

"Tunawashukuru sana Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe kwa ushirikiano wao mzuri, ambao umekuwa nguzo muhimu katika kazi zetu tangu tumeanza," alisema.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), zaidi ya asilimia 10 ya vijana duniani kote wanakumbana na matatizo ya afya ya akili, huku wengi wao wakikosa msaada wa kitaalamu mapema.

"Hapa Tanzania, changamoto hizi zimezidi kuongezeka kutokana na msongo wa mawazo, matumizi ya dawa za kulevya, ugumu wa maisha na unyanyapaa unaozunguka masuala ya afya ya akili kwa ujumla.

"Ni kwa sababu hii, Vanessa Amada Foundation imekuwa ikifanya kazi bega kwa bega na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ili kuhakikisha tunatoa suluhisho kwa changamoto hizi," alisema.

Alisema kwa miezi michache iliyopita, wamefanikisha kufikia zaidi ya vijana 3,000 kutoka vyuo vikuu vitatu na shule za sekondari tatu katika mkoa wa Dodoma kupitia programu yao ya AKILI.




Mkurugenzi wa Tiba wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Brigedia Jenerali Charles Mwanziva (kushoto) na Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Paul Lawala, wakionyesha nyaraka jijini Dodoma juzi, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya utoaji huduma za afya ya akili kati ya taasisi hizo. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Samia mgeni rasmi miaka 48 CCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya miaka 48 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo yatafanyika kitaifa jijini Dodoma Februari 5, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama hicho, Fadhili Maganya, alisema hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhalizi ya maadhimisho hayo kitaifa.

"Chama kitakuwa kinaadhimisha miaka 48 ya kuzaliwa kwake, sisi Jumuiya ya Wazazi ya CCM tumepewa jukumu la kuanza chereko chereko za sherehe hizi ambazo kilele ni Februari 5, mwaka huu, hapa Dodoma," alisema.

Alisema maadhimisho ya mwaka huu yataambatana na shughuli mbalimbali ikiwamo kongamano litakalofanyika Februari 2, mwaka huu, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete ambalo litakutanisha watu 3,500.

"Tutakuwa na kongamano ambalo limelenga kuleta watoa mada mbalimbali wasomi, viongozi, makada, na wanajamii ambao watazungumzia mahali ambapo chama kimetoka, kilipo na kinapokwenda," alisema.

Alisema, wataalamu hao watakuwapo wachokoza mada akiwamo Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi na wajadili mada mbalimbali, huku akiwaomba wanaDodoma na watanzania kufuatilia kongamano hilo.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Ally Hapi, alitaja baadhi ya mada zitakazowasilishwa katika kongamano hilo kuwa ni malezi, kuona chama kimechangiaje katika kujenga misingi ya maadili ya taifa, utamaduni na mila na desturi za Watanzania.

Mada nyingine ni mchango wa CCM katika maendeleo ya taifa katika kujenga umoja, mshikamano, uzalendo na maendeleo ya watu.

Aidha, mada kuhusu mchango wa Rais Samia katika kujenga chama na taifa, mchango wa vijana na elimu katika maendeleo ya taifa na mchango wa CCM katika kukuza misingi ya demokrasia nchini.

"Demokrasia yetu imetoka wapi, mchango wa CCM katika kujenga misingi ya demokrasia ikoje...hivyo mada zote zitaogelea ndani ya miaka 48 kwa maana ya majukumu ya chama ndani ya chama na chama kimefanya nini kwa wananchi na maendeleo ya taifa," alisema.





## Othman ataja mbinu uwezeshaji wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema maendeleo ya nchi ni kuwawezesha wananchi kutumia rasilimali zilizopo katika kupambana na kuondokana na umaskini kama zinavyofanya nchi mbalimbali duniani.

Othman aliyasema hayo jana katika viwanja vya Shule ya Mauwani, Jimbo la Kiwani Wilaya ya mkoani Pemba alipohutubia mkutano wa hadhara kwa wananchi na wafuasi wa chama hicho kuelezea masuala mbalimbali kuhusu umuhimu na mwelekeo wa uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema kuzitumia rasilimali za nchi na serikali kutokufanya kazi yenye tija kwa wananchi ni moja ya mambo yanayochangia kutopatikana ufanisi na nchi kukosa maendeleo ya kiuchumi na kijami, hivyo wananchi kuendelea kuwa maskini.

Alisema mataifa yote yanayopiga hatua za haraka kimaendeleo, maendeleo yanachangiwa na uwajibikaji wa wananchi na pia viongozi wa serikali kuwajibika na wananchi kuwa na uwezo wa kuwawajibisha viongozi waliowachagua.

Othman alisema chama chake kinaamini kuwa maendeleo ni kuwajenga watu na kuwawezesha wananchi katika masuala mbalimbali ya kupambana na umaskini, hivyo ndivyo ilivyofanyika katika yaliyopiga hatua.

Kuhusu karafuu, Othman alisema Zanzibar ina uwezo wa kurudisha uzalishaji mkubwa wa zao hilo hadi kufikia kiasi cha tani 30,000 kutoka wastani wa tani 7,000 hadi 8,000 kwa mwaka na kwamba uwezo huo upo iwapo uzalishaji utasimamiwa na serikali.

Alisema karafuu ni utajiri mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuwa ina uwezo wa kupanda bei na kuuzwa kwa zaidi ya Sh. 13,000 kwa kilo na tani 8,500 kuuzwa katika soko la dunia.

Pia alisema kinachohitajika ni serikali kuwezesha mfuko wa karafuu ili wakulima wakope na kuimarisha nyenzo katika uzalishaji wa zao hilo hatimaye kuwa na tija kwa wakulima na taifa kwa jumla.

Alisema zao hilo ni neema kubwa ambalo linaweza pia kuchukuliwa sambamba na minazi , zao ambalo halijasimamiwa ipasavyo na kuwa na tija kwa wananchi.

Alisema mataifa mbalimbali yanalitumia zao la nazi si tu kama rasilimali ya kupikia lakini kuna utaalamu wa aina mbalimbali wa kuliwezesha kuzalisha maradufu na kuwa na tija zaidi kwa matumizi mbalimbali.

# Kipenga uandikishaji wapigakura chapulizwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UANDIKISHAJI wa daftari la wapigakura wapya kwa awamu ya pili na ya mwisho kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu unatarajiwa kuanza leo visiwani Zanzibar.

Kazi hiyo itadumu kwa wiki mbili na itafungwa Machi 17, mwaka huu na itaanzia katika wilaya ya Micheweni, kisiwani Pemba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Vuga, mjini Zanzinar, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, alisema awamu ya kwanza walioandikishwa katika daftari walikuwa 57,883.

Waziri alisema kwa awamu ya pili, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inakadiria kuandikisha wapigakura wapya 78,922 waliotimiza umri wa miaka 18 kwa mujibu wa takwimu ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Alisema serikali haitaacha kumchukulia hatua za kisheria mwananchi yeyote atakayesababisha uvunjifu wa sheria katika kituo chochote cha kuandikisha wapigakura wapya.

Hamza alisema serikali imejiandaa kudhibiti uvunjifu wa amani au mtu yeyote atakayemzuia mtu kwenda kujiandikisha katika daftari la wapigakura.

Pia alisema mtu mwenye haki anapozuiwa kwenda kujiandikisha na kutengenezewa mazingira ya kutofika katika kituo ni sehemu mojawapo ya uvunjifu wa amani.

> **Pia alisema mtu mwenye haki amapozuiwa kwenda kujiandikisha na kutengenezewa mazingira ya kutofika katika kituo ni sehemu mojawapo yac uvunifu wa amani.**

Aliwataka wananchi wakihisi kuna hatari ya uvunjifu wa amani, kutosita kutoa taarifa katika kituo cha polisi kilicho karibu na hata ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili jambo hilo lidhibitiwe haraka.

Waziri alisema kazi hiyo itawahusu wapigakura wapya waliotajwa katika kifungu cha 12 cha Sheria ya Uchaguzi Na. 4 ya mwaka 2018 ambayo inamtaka Mzanzibari aliyetimiza miaka 18 na ataonesha kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi.

Sifa zingine, alisema ni kuwa mkazi wa kudumu na awe ameishi katika jimbo husika kwa kipindi cha miezi 36 mfululizo, asiwe katika daftari lolote la mpigakura na awe hazuiliki kuandikishwa kuwa mpigakura katika shehia nyingine.

Waziri Hamza alisema ni vyema wananchi wakajitokeza katika maeneo yao kwa amani na utulivu na kujizuia kuwa chanzo cha vurugu katika vituo vya uandikishaji na kutojaribu kuwazuia wananchi wengine wenye sifa ya kuandikishwa na kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa kifungu cha 118 (1) (b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Alisema sheria ya uchaguzi inatoa nafasi kwa kila chama cha siasa kuweka wakala kwenye kituo cha uandikishaji katika kila kituo ili kukiwakilisha na kugundua wanaojinufaisha.

Pia alisema wakala ana wajibu wa kushirikiana na karani wa uandikishaji katika kituo cha kujiandikisha kuhakikisha utekelezaji mzuri wa sheria kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 25 (1) hadi (3) (4) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar.

"Tanzania kuna vyama 19 ambavyo vimesajiliwa na kila chama kitapata fursa ya kusimamia katika uandikishaji huo," alisema.

Hata hivyo, alisema Sheria ya Uchaguzi katika kifungu cha 19 (1) (2) kimetoa nafasi kwa wananchi wanaohusika kuliwekea pingamizi jina lolote la mpigakura ambaye wanahisi ana sifa wakati wa uwekeji wazi wa orodha ya wapigakura walioandikishwa kazi ambayo hufanyika siku saba baada ya kukamilika uandikishaji katika shehia husika.

Pia alisema katika uandikishaji huo, uongozi wa wilaya haitasita kumuondoa mtu yeyote katika orodha ya walioandikishwa ambaye amewekewa pingamizi na kuthibitika kuwa hana sifa za kuwaandikisha kuwa mpigakura kwa kufuata utaratibu wa sheria uliowekwa.

Aliwataka waliotimiza sifa kujitokeza kwa wingi katika vituo vya uandikishaji ili kuandikishwa kuwa wapigakura na kuwaomba wananchi waendelee kutunza tunu ya amani iliyopo nchini kwa kuwa kufanya hivyo pia watakuwa wanatekeleza kaulimbiu ya uchaguzi mkuu ya mwaka huu iliyotolewa na ZEC isemayo 'kura haki yako, amani ni wajibu wako'.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, wakati akitangaza ununuzi wa Benki ya Canara Tanzania ambayo rasmi inakuwa sehemu ya benki ya Exim Tanzania. Ununuzi huo ni wa tatu kufanywa na benki hiyo ndani ya miaka sita iliyopita ikiwa ni sehemu ya juhudi zake katika kuboresha sekta ya kibenki ndani na nje ya nchi. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Fedha, Shani Kinswaga na Mkuu wa Idara ya Uwekezaji Kimkakati, Sumit Shekhar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi daraja kuongeza kasi maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo Chama cha Mapinduzi (CCM), Amos Makala, amesema ujenzi wa daraja la Kisiwa cha Uzi unaoendelea utaongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi wa kisiwa hicho. Makala aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo visiwani Zanzibar ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM.


Alisema wananchi wa kisiwa hicho watakuwa salama na kusafiri muda wote katika kushiriki shughuli za kijamii, kiuchumi na kimaendeleo.

Alisema ujenzi huo unaweka historia kubwa ya kuwa na daraja refu lenye kilomita sita ambalo litaunganisha wananchi wa kisiwa hicho na vijiji vyengine. Uzi ni miongozi mwa visiwa 52 vilivyoko Zanzibar na kimezungukwa na bahari na kina makazi ya wananchi 4,233.

Makala alisema dhamira ya CCM ni kuwaletea wananchi maendeleo na pia dhamira ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ni kutatua kero za wananchi.


Naye Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alisema mkoa huo unafunguka kiuchumi kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Mwinyi. Alisema katika uongozi wao, mkoa wa Kusini umepata miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kwenye sekta za maji, barabara, afya, elimu na uvuvi.

Alisema ujenzi wa daraja la Uzi unatarajiwa kumalizika kujengwa Septemba, mwaka huu na serikali pia inatarajia kujenga daraja la Charawe hadi Chwaka katika mkoa huo.



KOPA
UKURASA 12





# SAWA KAONDOKA, lakini jitafakarini

UNAWEZA kusema bundi anaendelea kuleta giza katika lebo ya muziki ya WCB, baada ya kuonekana dhahiri hali si shwari tena ndani ya taasisi hiyo inayolea vipaji vya wanamuziki.

Kuthibitishwa kuondoka kwa mwanamuziki pendwa Mbosso, inaonyesha kumekuwapo na vuguvugu kubwa la kuondoka kwa baadhi ya wasanii kutokana na sababu mbalimbali.

Kabla ya Mbosso, msanii mwingine kutoka lebo hiyo, Zuchu, ameonyesha dalili ya kuachana nao hasa baada ya kutokuwapo kwa maelewano na mpenzi wake Diamond Platnumz ambaye bosi wa lebo hiyo.

Baadhi ya wadau wa muziki wanaeleza vuguvugu la kuondoka kwa wasanii hao inaonyesha kwamba wanaona wamechoshwa na hali ilivyo kwa uongozi wa WCB.

Ieleweke wazi wasanii wote hao wana majina makubwa na watu wanaamini umaarufu wao uendane na kipato chao cha kila siku na kama ni tofauti itakuwa sababu ya wasanii kuamua kujiengua ili kwenda kutafuta maisha mengine.

"Kama wasanii wanakuwa maarufu na hawapati manufaa kulingana na kile wanachokiona, ni wazi kutaibua mgogoro na wengine kuamua kujiondoa. Lazima WCB waangalie kwa makini nini kinachofanya wasanii kuondoka kwa mkupuo," amesema Kilina Shamte.

Amesema hata kama uongozi wa WBC umempa baraka zote Mbosso kuondoka, lazima wajitafakari sababu ya msanii huyo kuwaacha baada ya kumlea kwa muda mrefu hadi kuupata umaarufu.

"Wengi wanaupongeza uongozi wa WCB kumuacha Mbosso aondoke bila mikwaruzano, lakini waangalia mapungufu ambayo wanaona ni chanzo cha wasanii kutotulia ili kuupata mwarobaini wake," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Darasa kageuka mfalme



RAPA mwenye mistari migumu, Darasa, anarejea katika mwonekano mpya akielezea albam yake italeta tofauti kati ya kazi zenye mashaka na zile zinazokubalika na jamii.

Darasa ambaye anaandaa uzinduzi wa albamu yake mpya inayoitwa Slave Become a King, yenye ngoma 15, atakuwa ni mara yake ya kwanza kutoa kazi tangu awe kimya kwa muda mrefu.

Ndani ya albumu hiyo kuna wanamuziki kadhaa mastaa walioshirikishwa wakiwamo Ali Kiba, Harmonize, Mbosso, Jay Melody na Bean wa Sauti Sol.

## Umelisikia debe la Jol Master?



MCHEKESHAJI wa jukwaani, Jol Master, amesema Mungu anampambania kumweka katika daraja la wasanii wakubwa wa fani hiyo nchini.

Amesema kutokana na kipaji alichonacho kwa sasa anaamini ameshika nafasi ya kwanza katika tasnia ya ucheshi kutokana na kuwa na kazi nyingi zenye ufanisi wa hali ya juu.

"Watanzania hawataki mtu kujisifia, lakini binafsi naamini nipo namba moja kuliko wachekeshaji wengine hapa nchini. Mimi pekee ndiye nafanya shoo peke yangu na kujaza ukumbi na kupata kazi nyingi kuliko wengine," amesema Jol Master.



# KOPA AWAKOSOA ZUCHU, DIAMOND

MALKIA wa taarab, Khadija Kopa, amesema wasanii wengi wa muziki wa kizazi kipya wakipanda jukwaani wanapiga kelele kuliko kuimba na kuburudisha wasanii.

Amesema kutokana na tatizo hilo kila mara anawatoa makosa Diamond Platnumz na Zuchu wakati wanapotumbuiza jukwaani na kuwataka wabadilike.

"Diamond na Zuchu huwa nawakosoa pale wanapotoka jukwaani kutumbuiza nawaambia wanapayuka ovyo, hawaimbi na hivyo wanatakiwa kubadilika waimbe wasifuate mayowe ya mashabiki watapotea," amesema Khadija.

FILAMU

# Kwetu Uswazi, balaa wazi wazi

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA jamii yetu wakati mwingine kuna mambo ya ajabu sana. Hii huwezi kusema uswahilini tu. Ni kwamba kuna vitu ambavyo mtu akikusimulia unaweza ukadhani kuwa ni hadithi tu na hazina ukweli wowote.

Kwenye filamu hii ya 'Kwetu Uswazi' kuna vitu ambavyo vinaweza kukuacha mdomo wazi, ukadhani kuwa ni mtunzi tu ameongeza chumvi. Lakini ni kweli kwenye baadhi ya jamii zetu kuna vitu kama hivi vinatokea.

Filamu hii imechanganyika na ucheshi kidogo kutokana na aina ya waigizaji aliogiza kama kina mzee Majuto na mzee Jengua ambaye wote ni marehemu. Pia kwenye filamu yupo mzee Msisiri.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa mzee Majuto na kijana wake Kinye Mkali wakizozana kutokana na wote kuwa na tabia mbaya ya kuchukua wanawake hovyo.

Imefikia wakati wanawake wa mzee Majuto ndiyo hao hao wa kijana wake Kinye Mkali, hivyo kuanza kuzozana wenyewe kwa wenyewe.

Jirani yao mmoja mlevi anafika nyumbani kwa mzee Majuto na kumuonya juu ya kutembea na mkewe.

Mkewe Majuto naye anakwenda nyumbani kwa mke wa mlevi huyo na kumpiga mkwara juu ya kutembea na mumewe.

Upande wa pili nako, mzee Msisiri ana wake wawili. Lakini wake zake hao wote wana uhusiano wa kimapenzi na kijana wa mzee Majuto, Kinye Mkali.

Habari hizo ikafika mpaka kwa mzee Msisiri mwenyewe kwa sababu walikuwa wakigombana mara kwa mara juu yake, na akaapa kumfanyia kitu kibaya.

Kwa mzee Jengua nako, wanaume kibao wanajitokeza kutaka kumposa binti yake, lakini anakataa.

Vijana wa kiume wakifika hapo, yeye anawatoa mbio.

Ikaja kufahamika kuwa mzee huyo ana uhusiano wa kimapenzi na binti yake.

Binti akaanza kuwa na kiburi kwa mama yake, huku mama akiwa hajui ni kwa sababu gani.

Siku moja shemeji wa mzee Jengua ambaye ni kaka wa mkewe, akawafuma laivu wakikumbatiana, akawa amepata jibu la kwa nini hataki binti aolewe.

Mzee Msisiri anamfanyia mambo ya kishirikina Kinye Mkali na anaanza kuwa chizi.

Matatizo ya akili ya mtoto wa Majuto yanasababisha wake za mzee huyo kumrudia mumewe na kumuoma msamaha. Ni kwa sababu hawawezi tena kuwa na uhusiano na mtu mwenye afya ya akili.



Mzee Msisiri aliwasamehe wake zake na kuwaruhusu kurejea nyumbani.

Shemeji wa mzee Jengua anakwenda polisi kushtaki kuwa mzee huyo anatembea na binti yake, kiasi cha kutakaa asiolewe.

Askari wanafika nyumbani na kumkatana mzee huyo na kupelekwa kituoni kwenye kujibu tuhuma hizo.





# Ukweli wa Mbosso kutoka WCB

MWANAMUZIKI na mtangazaji Baba Levo, amethibitisha kuwa msanii kutoka lebo ya WCB, Mbosso, ameondoka kwenda kuanza maisha mapya sehemu nyingine.

Amesema Mbosso ameondoka akiwa na baraka zote za bosi wake, Diamond Platinum, ikiwa pamoja na kumwachia kila kitu ambacho anaona kitamsaidia akiwa nje la lebo hiyo.

"Diamond hana shida na pesa ndio maana kamwachia Mbosso kila kitu ikiwamo mamlaka ya kuendesha akaunti zake za mitandao ya kijamii kutokana na nidhamu yake. Mbosso katoka vizuri kuliko wasanii wengine huko nyuma," amesema baba Levo.

# WANAMUZIKI WASIOHAMA BENDI

**Na Adam Fungamwango**

Leo tuna wanamuziki ambao walikuwa na roho ngumu. Walikuwa wagumu kuhama kwenye bendi zao licha ya kwamba kulikuwa na majaribio kadhaa ya kutaka kuwachukua, lakini wakang'ang'ana hapo hapo na sababu kubwa ilikuwa ni kutotaka kuwakera na kuwaudhi mashabiki wao, lakini pia wengine walizuia.

### Tx Moshi William-Msondo Ngoma

Ni mwanamuziki kipenzi kabisa cha wana Msondo Ngoma ambaye hawakukubali hata chembe ahame.

Mashabiki wa Msondo walitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha haondoki na walifanikiwa hadi Mwenyezi Mungu alipomchukua mwaka 2006, ndipo waliposhindwa kufanya chochote.

Alikaa kwenye bendi ya Msondo kwa miaka 24 bila kuhama, ingawa kulikuwa na majaribio ya hapa na pale yaliyoshindwa.

Katikati ya miaka ya '80 akiwa anakaribia kutambulishwa kwenye onyesho la DDC Mlimani Park ukumbi wa DDC Kariakoo, alinyakuliwa kama kifaranga na mashabiki wake waliovamia hapo na kukodi Taxi, kumpeleka kwenye ukumbi wa DDC Keko ambako Msondo walikuwa wakifanya onyesho.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, TOT Plus ilikaribia kumnyakua baada ya kumpa gari na kumvutia maji nyumbani kwake, lakini wadau wa Msondo walizima jaribio kwa kurudisha gharama zote na pia kumnunulia gari lingine.

### Nasri Lubua-DDC Mlimani Park

Ni mwimbaji wa sauti ya kwanza aliyejiunga na Sikinde kutoka Lola Africa mwaka 1985 kuziba nafasi ya Hassan Rehani Bitchuka aliyekuwa ametimkia Orchestra Safari Sound (OSS) ya mtindo wa Ndekule na baadaye kurudi Msondo.

Nasri ambaye awali alijulikana kwa jina la Francis Lubua aliendelea kukaa kwenye bendi hiyo hadi alipofariki dunia mwanzoni mwa miaka ya 2000.

### Abdul Ridhwani -Msondo Ngoma

Ni maarufu zaidi kwa jina la Pangamawe. Ni mpiga gitaa la solo kwenye bendi ya Msondo Ngoma. Alijiunga na bendi hiyo akiwa na umri wa chini ya miaka 3 mwaka 1980 akiwa kama mpiga kinanda baada ya kuondoka kwa Waziri Ally kwenda kuanzisha bendi iliyokuja kujulikana zaidi kwa jina la Njenje.

Baadaye akahamia kwenye gitaa la bass kwa muda mfupi, lakini akageuka kuwa mpiga gitaa la solo wa kutegemewa, akirithi mikoba ya Kassim Mponda baada ya kuihama bendi hiyo na kwenda Sikinde. Hadi leo ni miaka 39, bado yuko na bendi hiyo akiendelea na kazi ya muziki.

### Habib Abbas-DDC Mlimani Park

Ni mmoja wa waanzilishi wa bendi ya Mlimani Park Orchestra mwaka 1978. Wanamuziki wote waanzilishi, walitoka kwenye bendi hiyl wengine wakarejea na wengine wamefariki dunia, lakini Habib Abbas Jeff Mgalusi yeye bado yupo na bendi hiyo hadi leo. Ni mpiga drums tegemeo wa bendi hiyo aliyejiunga akitokea bendi ya Afro 70 ya Patrick Balisidya. Ameitumikia bendi hiyo kwa miaka 43 sasa.

### Said Mabera-Msondo Ngoma

Ndiye mwanamuziki aliyeweka rekodi ya kukaa kwa muda mrefu kwenye bendi moja nchini mpaka sasa. Alikaa Msondo kwa miaka 46, hadi mwaka 2020 alipofariki dunia.

Alijiunga na bendi hiyo mwaka 1974 akitokea National ya Arusha akiwa na Bitchuka. Awali Mabera alikuwa akipiga trumpet, lakini aligeuka kuwa mpiga solo namba moja wa bendi hiyo, na hiyo ni baada ya kuchukua mikoba ya Abel Bathazal aliyeiacha bendi na kwenda kuunda Dar Intenational mwaka 1977.

# Genevieve, Flavour hawapoi

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Genevieve Nnaji na mwanamuziki maarufu, Flavour N'abania, hivi karibuni wameibua gumzo baada ya kuonekana wakiwa pamoja.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Flavour ambaye ana miaka 41, alichapisha video inayowaonyesha wawili hao wakibarizi pamoja katika sehemu moja tulivu.

Hata hivyo, mashabiki wengi wanahoji umri wa Genevieve kumzidi Flavour kwa miaka minne wakieleza utakuwa kikwazo katika uhusiano wao.





## Khanyi amtuliza Annie

MSANII wa filamu na mwanamuziki nyota wa Afrika Kusini, Khanyi Mbau, amejitokeza hadharani kumuunga mkono Annie ambaye alikuwa mke wa mwanamuziki wa Nigeria 2baba, baada ya kupewa talaka.

Kupitia kurasa yake ya Instagram, Mbau alisema taarifa hiyo ilimfanya kuwa mgonjwa na kumtuhumu 2baba kwa kukimbilia mitandao ya kijamii katika masuala ya ndani.

"Hakuna kinachonifanya niwe mgonjwa kama mwanaume anayekimbilia mitandao ya kijamii pale mambo yanapokwenda mwisho katika uhusiano wake. Annie mwacheni atembee peke yake," ameandika.

## Burna Boy fedha zinaongea

MWANAMUZIKI maarufu kutoka Nigeria, Burna Boy, amezidi kuonyesha jeuri ya fedha baada ya hivi karibuni kuonekana akiwa amevaa saa za bei mbaya za mkononi.

Saa hizo ambazo zinavaliwa na mastaa matajiri Richard Mille na Patek Philippe, zinajulikana kuwa na gharama kubwa na hivyo Burna Boy atakuwa miongoni mwa wasanii wachache wanaozimiliki.

Katika video aliyoweka katika mtandao wake wa Instagram, gwiji huyo wa muziki wa Afrobeats, alionekana akiwa amevaa saa mbili kwenye mikono yake yote miwili huku akitabasamu.





## Tee Billz kamaliza ya moyoni

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, Tee Billz, amemuonya mwigizaji Toke Makinwa, kuwa mbali na familia yake na kwamba hana sifa ya kusamehewa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Billz amesema Toke bado hajafikia kiwango cha kupewa msamaha na upendo ambao wanawake wengine kama mke wake wa zamani, Tiwa Savage wanayo.

"Toke Makinwa kuwa na mtoto kwa ajili ya mwanamume ni aina tofauti ya msamaha na upendo ambao bado hujaupata. Naomba ufanye dada," ameandika Billz.

## Tems aikacha Rwanda

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Temilade Openiyi maarufu kama Tems, amefuta onesho lake nchini Rwanda lililopangwa kufanyika Machi 12, kutokana na mgogoro kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda.

Tems ameandika kupitia ukurasa wake wa X, kuomba radhi mashabiki zake kutokana na kitendo chake cha kuendelea kuandaa onyesho lake hilo bila kufahamu kuwa kuna mzozo unaoendelea kati ya nchi hizo mbili.

Tems ametoa pole kwa wote walioathirika na vita hiyo na kueleza anaomba Amani ipatikane.





# DC afuta viwanja 180 kisa utapeli

**Na Allan Isack,** MONDULI

MKUU wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga, amevifuta viwanja 183 vinavyodaiwa kuuzwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Moita Bwawani, Bruno Joseph, bila kufuata utaratibu.

Uamuzi huo unatokana na mwenyekiti wa kijiji hicho, kuuza viwanja na kuchuchukua fedha kinyume na utaratibu.

Akizungumza na wakazi wa kijiji hicho jana, alipokwenda kusikiliza na kutatua mgogoro uliodumu kwa takribani miaka minne, Kiswaga alisema amerudisha viwanja kwa wananchi kwa ajili ya kupangiwa utaratibu mwingine wa namna ya kuvitumia hasa kwa malisho ya mifugo.

Mkuu huyo wa wilaya pia aliagiza watu waliojenga kwenye maeneo waliyouziwa kuondoka ndani ya wiki moja na kuyaacha kwa ajili ya malisho ya mifugo.

"Watu walioko kule na waliojenga waondolewe mara moja. Ninawapa wiki moja kuhamisha vitu waondoke kwa kuwa maeneo hayo yametengwa kwa ajili ya malisho ya wananchi wa kata ya Moita," alisema.

Aidha, alisema kiongozi huyo wa kijiji alipouza viwanja hivyo alishindwa kuziweka fedha kwenye akaunti ya Kijiji, kinyume cha sheria, kanuni na utaratibu wa serikali.

**"Mwenyekiti wa kijiji pamoja na wenyeviti wa vitongoji wote mnapaswa kufahamu kuwa jembe la busara halipo tena, limefutwa kuanzia sasa na watu waliojenga huko waondolewe mara moja," alisema Kiswaga.**

"Kuanzia leo (jana) nafuta rasmi jembe lililokuwa linaitwa la busara kwa kuwa lilikuwa la wizi na asije akajitokeza mtu yeyote akasema ana shamba, kiwanja au ana haki. Kule ni marufuku eneo hilo kutumika kwa kuwa limetengwa kwa shughuli za malisho ya mifugo. "Mwenyekiti wa kijiji pamoja na wenyeviti wa vitongoji wote mnapaswa kufahamu kuwa jembe la busara halipo tena, limefutwa kuanzia sasa na watu waliojenga huko waondolewe mara moja," alisema Kiswaga.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Moita Bwawani, Joseph, alisema ameonewa kwa kuwa mkutano huo si wa kijiji hicho.

"Nimeonewa kwa kuwa mkutano huu si mkutano mkuu wa kijiji cha Moita Bwawani bali ni mkutano wa kata na mgogoro huu ni wa kijiji na ardhi hii ni yetu.

"Nikuhakikishie tu DC (Mkuu wa Wilaya) hawezi kufuta kwa kuwa ni uamuzi wetu ambao tulikubaliana wote na kikao hiki sio sahihi cha kutoa maamuzi na waliokuwa hapa kwenye mkutano huu walalamikaji ni wananchi kutoka vijiji vingine," alisema mwenyekiti huyo.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (mwenye miwani), akizungumza na maofisa wa Jeshi la Magereza, alipotembelea Gereza la Babati jana, kukagua utekelezaji wa matumizi ya nishati safi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# TAKUKURU yaokoa mamilioni ya chanjo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Manyara, imeokoa Sh. milioni 3.3 zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu na Mratibu wa Chanjo ya Surua na Rubella katika wilaya ya Mbulu.

Kwa mujibu wa Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Manyara, Bahati Haule, mratibu huyo ambaye jina lake limehifadhiwa kwa ajili ya taratibu za kiuchunguzi, alifanya ubadhirifu huo kwa kuongeza gharama za chakula cha washiriki 435 wa semina ya watoa huduma ya utoaji wa chanjo, baada ya kughushi stakabadhi za marejesho.

"Mratibu huyo alimwaminisha mwajiri wake, ambaye ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, kwamba ametumia shilingi milioni 6.525, wakati akijua mzabuni aliyefanya huduma hiyo alilipwa shilingi milioni 3.225," alisema Haule.

Aidha, TAKUKURU Mbulu imefanya uchunguzi na kubaini udanganyifu huo na Desemba mwaka jana, mtuhumiwa alirudisha fedha hizo pamoja na kuchukuliwa hatua nyingine za kinidhamu.

Wakati huo huo, TAKUKURU kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, imefuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo 20 iliyogharimu Sh. bilioni 9.765.

Vilevile, Haule, alisema miradi iliyofuatiliwa ni ujenzi wa miundombinu ya maji, ujenzi wa wodi za hospitali, ujenzi wa miundombinu ya barabara, ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za sekondari, ujenzi wa mabweni sekondari.

Pia iko miradi mitano yenye thamani ya Sh. milioni 435.8, iliyobainika kuwa na mapungufu, ambapo tayari hatua mbalimbali zimechukuliwa kukabiliana na mapungufu hayo.

# Wakutana kujadiliana upatikanaji wa nishati

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATAALAMU wa nishati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na wa sekta binafsi, wamekutana jijini hapa kujadiliana jinsi ya kuboresha upatikanaji wa nishati mbadala kwa gharama nafuu.

Mwakilishi wa Vijana katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA), James Magesa, akizungumza jana kwenye mkutano wa siku mbili wa Ushirikiano wa Nishati wa Afrika Mashariki (EA-ECS), alisema ni wakati muafaka sasa kwa nchi hizo kutumia nishati mbadala inayotokana na jua, upepo na makaa ya mawe. "Wataalamu wa nishati kutoka nchi za EAC na wadau wa sekta binafsi tumekutana hapa ili kujadiliana namna bora ya kuboresha uzalishaji wa nishati ya jua, upepo na makaa ya mawe ili utumike viwandani kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi wanachama," alisema.

Pia alisema wajumbe wa mkutano huo pia wanajadiliana namna bora yavkuwa na soko la pamoja la kuuziana nishati mbadala kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na kila mchi kuongeza uzalishaji wa nishati hiyo. "Katika mkutano huu pia tumejadiliana namna ambavyo tunaweza kutumia umeme wa Bwana la Mwalimu Nyerere linalozalisha Megawati 200 ili kuzisaidka nchi za EAC kupata umeme wa uhakika viwandani ambao utasaidia kuongeza ajira hasa kwa makundi ya vijana.

"Tumefanya mkutano huu sababu tumeona nchi nyingi za EAC hazina umoja katika masuala ya nishati ndio maana tunajaribu kuona jinsi ya kuwa na soko la pamoja ili kusaidiana kwenye nyanja hiyo sisi wenyewe wanachama,"alisema.

Mratibu wa mkutano huo, Abdoulaye Sylla, alisema lengo la kufanya mkutano huo ni baada ya kuona baadhi ya nchi za EAC zinafanya vizuri kwenye masuala ya nishati katika miaka michache iliyopita. "Nchi kama Tanzania, Kenya, Ethiopia na Uganda zinafanya kazi nzuri katika eneo la nishati mbadala, hivyo tunajaribu kukuza ushirikiano ili kuweka nguvu katika eneo hili," alisema.

Mkutano huo umekutanisha wazalishaji nishati binafsi Afrika na wadau wa uhandisi, manunuzi, ujenzi na fedha (EPCF), lengo ni kutathmini uwezekano wa uwekezaji na uvumbuzi ulioanzishwa na kampuni muhimu kimkakati, ikijumuisha vituo vya Data Afrika.

MAKALA

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Huyu ndiye aliyeigiza kama mlevi, wimbo 'Whisky Soda'

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 1970, kulikuwa na wimbo mmoja uliokuwa unasikika kwenye redio ulioshangaza watoto wengi wa wakati huo.

Natumai wakubwa hawakushangaa, lakini watoto wengi walionyesha kushangaa, kufurahi na kucheka kwa wakati mmoja kwani haikufanana na nyimbo ambazo wamewahi kuzisikia kabla.

Kusikia wimbo kwenye redio ambao unaimbwa na mlevi ni kitu ambacho kilionekana cha ajabu sana.

Watoto wengi walishangaa kuona mlevi anapewa nafasi ya kuimba, wakati anaimba 'kipombepombe.'

Pamoja na hayo, staili hiyo ya uimbaji iliwakosha watoto wengi na kufanya kuupenda wimbo huo.

Siyo kama walipenda maneno yake, bali aina tu ya uimbaji wa mlevi hiyo, ambaye kuna wakati kama anaimba, kuna wakati kama anafokea mtu, baadaye kama anataka kutapika, mara anamfukuza mtu au mnyama, yaani vituko baada ya vituko.

Watoto waliupenda sana na wala hawakuwa na haja ya kuuliza ulipigwa na bendi gani, ya wapi na hata mtunzi ni nani.

Watu wazima nao walitokea kuupenda sana kwa sababu ulikuwa wimbo ambao uliongeza ladha na ubunifu wa muziki, kwani ulitengenezwa tofauti na nyimbo zingine, huku katikati ya wimbo ukiimbwa na 'mlevi' huyo.

Inawezekana hadi leo hii kuna baadhi ya watu ambao wanaufahamu wimbi huo, lakini hawajajua ni bendi gani au ni mwanamuziki gani alitunga wimbo huo.

Kwanza kabisa, wimbi huo jina lake ni 'Whisky Soda.' Ulitungwa na kuimbwa na mwanamuziki raia wa Guinea, Aboubacar Demba Camara.

"Mano mambo, eeeh mano eee, mano whisky soda, mano mambo..." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.

Hata hivyo zipo taarifa kuwa mtunzi halisi wa wimbo huo ni Baba Soumano, raia wa nchi hiyo, ambaye alirekodi mwaka 1950.

Hata hivyo umaarufu wa wimbo huo, ulipatikana mwanzoni mwa mwaka 1970, Demba Camara, alipourudia akiwa na bendi ya Bembeya Jazz National.



Aboubacar Demba Camara.

Na yeye ndiye 'aliyeekti' kama mlevi, akiwavunja watu mbavu. Inasemekana hakuwa anakunywa pombe kabisa.

Nadhani wengi watataka kumfahamu kiongozi huyo wa bendi hiyo, ambaye mbali na wimbo huo, alijipatia umaarufu mkubwa miaka hiyo kwa nyimbo zake kama 'Mamiwata', 'Beni Barale', 'Ballake', 'Moussogbe', 'Tama Tama' na zingine nyingi.

Alizaliwa mwaka 1944 huko Conakry, Guinea ya Kifaransa katika familia kutoka Saraya. Alisoma katika shule ya msingi ya Coléa hadi mwaka 1952, alipohamia shule nyingine huko Kankan.

Mnamo 1957, alirejea Conakry kumaliza masomo yake ya msingi kabla ya kurudi Kankan, ambako alijiunga na shule ya ufundi na kupata cheti chake cha useremala. Mwaka 1963, alihamia mji wa Beyla kusini mwa Guinea kwa ajili ya kazi.

Demba Camara alijiunga na bendi ya Bembeya Jazz National mwaka 1963. Alikuwa kiongozi wake, mwimbaji mkuu, na mtunzi wa nyimbo. Katika kilele cha umaarufu wake, Demba Camara alitangazwa kuwa mwimbaji bora wa Afrika na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC).

Machi 1973, Bembeya Jazz National ilialikwa nchini Senegal na serikali ya Guinea kwa ajili ya ziara ya maonyesho. Bendi hiyo ilipokelewa kwa shangwe katika Uwanja wa Ndege wa Dakar-Yoff, Machi 31, ambapo waliondoka kwa msafara kuelekea mjini Dakar.

Katika makutano ya barabara mbele ya Deux Mamelles, gari aina ya Peugeot 504 lililombeba Demba Camara, mpiga gitaa wake Sekou Diabate, na mwimbaji Salifou Kaba lilipata ajali.

Demba Camara alinaswa chini ya mlango wa gari na akapelekwa hospitalini ya Dentec nchini humo pamoja na wenzake.

Madaktari waligundua kuwa alikuwa na ufa kwenye fuvu la kichwa, kifua, na majeraha kadhaa. Licha ya juhudi za madaktari, alifariki dunia, Aprili 5, 1973, kutokana na kutokwa na damu nyingi.

Baada ya kutangazwa kwa kifo cha Demba Camara, ujumbe wa serikali ya Guinea na kamati kuu ya Parti Democratique de Guinee, ukiongozwa na Waziri wa Elimu Mamadi Keita, ulisafiri kwenda Dakar kuchukua mwili wake.

Ndege yao ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Dakar-Yoff, ambako ilipokelewa na umati mkubwa wa waombolezaji na ujumbe wa serikali ya Senegal ukiongozwa na Rais wa Bunge Amadou Cisse Dia.


Alisema kuwa serikali ya Senegal haikuacha juhudi zozote katika kujaribu kumuokoa Demba Camara, lakini ilishindikana.

Waguinea walitua Conakry na mwili wa Demba Camara ukapelekwa Palais du Peuple kwa lori, ambako ulipokelewa na maelfu ya waombolezaji.

Rais wa wakati huo, Ahmed Sekou Toure, mke wake walipiga magoti mbele ya jeneza lake. Demba Camara alifanyiwa mazishi ya kitaifa, yaliyowakilishwa na wanachama wa serikali za Guinea na Senegal.

Watu laki moja waliovaa mavazi meupe walifuata mwili wake kwa maandamano kuelekea makaburi ya Camayenne, yakiongozwa na bendi ya jeshi la Camp Boiro iliyokuwa ikipiga wimbo wa Boloba, wa Manding unaochezwa kwa heshima ya mashujaa wa nchi tu.

**Tuma meseji 0716 350534**



HABARI KIMATAIFA

# MOTO WAZIDI KUWAKA DRC

## -Trump aitaja Rwanda tatizo
## -Vikosi vyasogezwa mpakani



Waasi wa M23 wakiwa mjini Goma. **PICHA: GETTY IMAGES**

**GOMA, DRC**

WAKATI viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) wakikutana nchini Zimbabwe kujadili mgogoro wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Rais wa Marekani Donald Trump, ameitaja Rwanda kuwa ni tatizo kubwa.

Akizungumza katika mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu ajali ya ndege jijini Washington, Rais Trump aliulizwa na mwandishi mmoja wa habari aliyetaka kujua kama Marekani ina mpango wa kwenda kurudisha amani nchini DRC.

Akijibu swali hilo, Trump alisema mgogoro huo ni tatizo kubwa, lakini hakutoa ufafanuzi kuhusu kauli hiyo.

"Unaniuliza kuhusu Rwanda, ni tatizo kubwa sana, nakubaliana na wewe lakini sidhani kama ni sahihi kwa sasa kulizungumzia jambo hilo. Lakini ni tatizo kubwa sana," alisema.

Rwanda imekuwa ikituhumiwa kuwasaidia waasi wa M23 ambao wameteka maeneo mengi mashariki mwa nchi hiyo. Hata hivyo, Rais Paul Kagame amekuwa akikanusha tuhuma hizo.

Aidha, wakuu wa nchi wanachama wa SADC wamekutana kwenye mkutano huo wa dharura ulioitishwa kwa lengo la kujadili hali ya ulinzi na usalama mashariki mwa DRC.

Mkutano huo umeongozwa na Rais Emmerson Mnangagwa, wa Zimbabwe, ambaye ni Mwenyekiti wa SADC.

Katika kikao hicho wakuu hao wa nchi wanachama wanatarajiwa kujadili hatua za kuchukua kumaliza mapigano katika eneo la mashariki mwa DRC, pia kutoa hatima ya operesheni ya kijeshi kwa vikosi vya SADC ambavyo viko katika eneo hilo.

Zimbabwe tayari imeonyesha wasiwasi wake kuhusu mapigano yanayoendelea DRC yataleta athari kwa nchi wanachama.

Wanajeshi kadhaa kutoka Afrika Kusini, Malawi na Tanzania wameuawa wakati walipokabiliana na waasi wa M23 kwa wakati tofauti.

Wakati huo huo, msemaji wa serikali ya Rwanda, Yolande Makolo, ameiambia BBC, nchi yake imepeleka vikosi vyake vya kijeshi katika maeneo ya kujihami na mashambulizi ili kuepuka kusambaa kwa mzozo huo mashariki mwa Congo.

Licha ya ushahidi unaoongezeka kwamba wanajeshi wake wanapelekwa kusaidia na kuongoza mashambulizi ya waasi wa M23, serikali ya Rwanda inaeleza hatua hiyo ni kudumisha usalama wa mipaka yake.

Makolo alisema watu wasiopungua 15 wameuawa nchini Rwanda kwa makombora kutoka DRC.

Uganda pia imechukua hatua kama hiyo kwa kutangaza kuimarisha ulinzi katika mpaka wake na DRC ili kuwazuia watu wenye silaha kuingia nchini humo.

Taarifa kutoka Wizara ya Ulinzi ya Uganda, ilisema vikosi

vitakuwa karibu na mji wa kaskazini wa Beni kwa ajili ya kujihami ili kuzuia makundi yenye silaha kutumia vibaya mgogoro huo.

Kwa upande mwingine nchi za Uingereza na Ujerumani ambazo ni wafadhili wakuu wa Rwanda zimetangaza kuchunguza upya msaada wao kwa nchi hiyo ambayo inatuhumiwa kuwaunga mkono waasi.

Zaidi ya asilimia 40 ya bajeti yake ya kitaifa inafadhiliwa kupitia misaada kutoka nchi za kigeni.

Hata hivyo, serikali Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo imetoa wito wa jumuiya ya kimataifa kuiwekea vikwazo Rwanda na kusitisha misaada ikiwamo kuondolewa ushiriki wake katika misheni ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC, aliiambia BBC, kwamba Rwanda inakalia eneo la nchi yake kinyume cha sheria.

Therese Kayikwamba Wagner alisema Rwanda inaunga mkono, kufadhili na kuandaa ujasusi ambao unatafuta njia ya kupindua serikali iliyochaguliwa kisheria.

Ikijibu madai hayo, msemaji wa serikali ya Rwanda alisema nchi yake inatetea mipaka yake wala haina nia ya mabadiliko ya serikali.

Viongozi wa waasi ambao walichukua udhibiti wa baadhi ya sehemu za Jiji la Goma wiki hii walisema Alhamisi kwamba wanakusudia kufika Kinshasa.

Msemaji wa serikali ya Rwanda alisema nchi yake haina nia ya mabadiliko ya serikali Congo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Noel Barrot, aliwasili nchini Rwanda kwa ajili ya mazungumzo na Rais Paul Kagame kuhusu suala la kumaliza vita mashariki mwa DRC, hayo ni kwa mujibu wa AFP. Barrot aliwasili juzi mjini Kigali akitokea Kinshasa ambako alikutana na Rais wa DRC, Rais Félix Tshisekedi.

Redio ya kimataifa ya Ufaransa, RFI, iliripoti kwamba Barrot alimweleza Rais Tshisekedi kwamba Ufaransa inaitaka Rwanda kuondoa wanajeshi wake mashariki mwa DR Congo, na kwamba M23 iondoke katika maeneo ambayo tayari imeyateka.

Tishio hadi Kinshasa

Wakati huo huo, kiongozi wa kisiasa wa kundi la waasi la M23, Cornelle Nangaa, ameapa kuwa wapiganaji wake hawatakubali kuuachia mji wa Goma.

Alisisitiza kuwa wataendelea kuidhibiti Goma na wataendelea na safari yao hadi katika jiji la Kinshasa kuondoa utawala wa Rais Felix Tshisekedi.

Taarifa hiyo ni ya kwanza tangu wapiganaji wa M23 kuchukuwa udhibiti wa mji wa Goma ambao unakaliwa na watu milioni tatu.

Nangaa ni kiongozi wa "Alliance Fleuve Congo, kundi la kisiasa na kijeshi linalotaka kuipindua serikali ya DRC. Katika mkutano na vyombo vya habari uliofanyika hotelini, Nangaa ambaye alivaa sare za kijeshi na alikaa katikati ya makamanda wa waasi.

Kiongozi huyo alitangaza mpango wa kuelekea mji mkuu wa Kinshasa, kwa lengo la kuipindua serikali ya Rais Félix Tshisekedi.

Nangaa alieleza wazi kuwa waasi sasa wanatawala Goma na katika saa 48 zijazo, kazi itaendelea ya ujenzi wa Goma, ikiwamo kufunguliwa kwa shule.

**BBC, DW**

# Bodi ya Korosho kuzalisha tani 1,000,000 ifikapo 2030

Na Joseph Mwendapole

BODI ya Korosho (CBT), imesema ingawa uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani 310,000 msimu wa 2023/2024 mpaka kufikia tani 410,000 msimu wa 2024/2025 lengo lake ni kuongeza uzalishaji huo hadi kufikia tani 1,000,000 mwaka 2030.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Francis Alfred wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano mkubwa unaotarajiwa kuwakutanisha wadau 500 wa uzalishaji wa zao la korosho jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo wa 19 uliaondaliwa kwa pamoja baina ya Bodi ya Korosho Tanzania na Jukwaa la Korosho Afrika (African Cashew Alliance), utafanyika nchini kwa mara ya tatu Novemba 18 hadi 22 na mara ya kwanza ulifanyika mwaka 2007 na mara ya pili mwaka 2009.

Alisema ili kufikia lengo la kuzalisha tani 1,000,000 kwa mwaka Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na bodi hiyo wameajiri vijana 500 kupitia mpango wa jenga kesho iliyobora (Building Better Tommorow BBT).

Alisema jukumu la vijana hao ni kutoa huduma za ugani kwa wakulima pamoja na kusimamia shughuli mbalimbali za uendelezaji wa zao hilo katika kata zote zinazolima korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga.

Alisema ili kufikia lengo la kubangua korosho zote zinazozalishwa hapa nchini ifikapo mwaka 2030, serikali imetenga eneo la ekari 1,572 kwa ajili ya mradi wa kongani ya viwanda katika kijiji cha Maranje mji wa Nanyamba Mtwara.

Alisema kongani hiyo inatarajiwa kuwa na viwanda 30 vya kubangua korosho, viwanda sita vya kukamua mafuta ya ganda la korosho na viwanda vinne vya kusindika ufuta.

Kuhusu mkutano huo, alisema utasaidia kufungua fursa za uwekezaji kwenye sekta ya korosho na kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko kwenye tasnia hiyo kuanzia shambani ambapo wanatarajia kupata wawekezaji wakubwa kwenye mashamba ya korosho.



Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho (CBT), Francis Alfred (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano wa wadau wa korosho duniani unaotarajiwa kufanyika katika jiji hilo, Novemba 18 mwaka huu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

Alisema mkutano huo utahudhuriwa na washiriki 500 kutoka nchi zote mbalimbali duniani zikiwamo 33 zinazolima korosho na kutaja baadhi ya nchi hizo kuwa ni Ivory Coast, Cambodia, India, Vietnam, Brazil, Indonesia, Sri Lanka, Nigeria, Guinea Bissau na Burkina Faso.

Alitaja zingine kuwa ni Mali, Benin, Ghana, Madagascar, Zambia, Msumbiji, Kenya, Mauritius, Visiwa vya Comoro na wenyeji Tanzania.

Alisema mkutano huo pia utawashirikisha wadau wa nchi zinazoongoza kwa ulaji wa korosho kama Marekani, Ulaya, China, Uarabuni, Afrika Kusini, Mashariki ya Kati na nchi zingine za Bara la Afrika.

Alisema mkutano utawashirikisha wadau walioko kwenye mnyororo wa thamani wa tasnia ya korosho kama vile wakulima, wabanguaji, wasindikaji, wakaangaji, wasafirishaji, vyama vya ushirika na wasambazaji.

Alisema matarajio ni kuongeza ubanguaji wa korosho ambapo viwanda vya kubangua na kusindika korosho na bidhaa zake vitaongezeka ndani na nje ya nchi za Afrika.

"Kwa upekee mkutano huu utatumika kuhamasisha matumizi ya korosho na bidhaa zake kama vile mafuta ya maganda ya korosho (cashewnut shell liquid, maziwa ya korosho na pombe kali," alisema.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya sita imefanya juhudi kubwa za kuendeleza zao hilo ambapo kwa miaka mitatu sasa imekuwa ikitoa ruzuku ya

# RC ataka viongozi kuwa na shamba darasa ili wananchi wajifunze kwao

Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amewaagiza viongozi wote mkoani humo wawe na shamba ili wananchi wajifunze kwao, badala ya kuwahimiza kulima wakati hawana mashamba.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha kupata taarifa kuhusu mgao wa mbegu za alizeti zenye ruzuku ambazo zimepelekwa mkoani Singida.

Kikao hicho kiliwashirikisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wenyeviti wa halmashauri na maofisa kilimo.

"Tusiwe tunaimba wimbo wa kilimo wakati sisi wenyewe hatulimi. Tukubaliane hapa kuanzia mkoani, wilayani hadi kwenye kata, kila mmoja angalau awe na shamba la ekari moja, litakuwa shamba darasa kwa wananchi kufika kujifunza, waone mbolea na mbegu zinavyofanya kazi," aliagiza.

Dendego aliagiza mbegu za alizeti zilizoletwa mkoani humo zikishafika wilayani zisambazwe haraka kwa wakulima ili kilimo cha zao hilo kiweze kuanza mara moja.

Aliwataka viongozi wa wilaya zote kuendelea kuwahamasisha wananchi kulima ili kiwango cha uzalishaji wa alizeti kiongezeke katika msimu huu, kwani Mkoa wa Singida unategemewa kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya alizeti.

Alisema katika msimu wa kilimo mwaka huu, mkoa umepanga kulima ekari 1,025,641 za alizeti na kupata mavuno tani 1,000,000.

Dendego alisema kulingana na ekari hizo zinazotarajia kulimwa, kunahitajika mbegu za alizeti tani 2051 ambapo mpaka sasa kwenye halmashauri, kuna tani 101.814 mbegu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga, alisema serikali iangalie namna ya kulegeza masharti ili wananchi ambao hawana fedha taslimu wakopeshwe na kulipa baada ya kuvuna mazao.

# Elimu ya kodi yaongeza ukusanyaji wa mapato

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, utoaji wa risiti za mauzo na ununuzi wa bidhaa na huduma ikiwamo ya kutoa elimu ya kodi.

Chande alisema hayo Bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Janeth Mahawanga, aliyetaka kujua mpango wa serikali wa kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kudai risiti.

Chande alisema kuwa elimu ya kodi inatolewa kwa njia ya redio, runinga, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho ya biashara ya kitaifa, kimataifa na semina.

Alisema serikali inawatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao mlango kwa mlango kutoa elimu inayoainisha wajibu wa mlipakodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wajibu wa TRA kwa mlipakodi kupitia Mkataba wa Huduma kwa Mlipakodi.

"Tumeanzisha huduma za bure ikiwamo namba za simu za bure zinazowezesha walipakodi kuwasiliana na ofisi za TRA na tumeanzisha ofisi zinazotembea (mobile tax offices) ambazo zitatumika kama ofisi kamili kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi kwa umma na kusajili walipakodi wapya," alieleza Chande.

Akieleza kuhusu kuboresha mfumo wa kutoa risiti, Chande alisema serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya mlipakodi na kudhibiti mapato ya serikali kwa kuweka msisitizo wa kuhakikisha mifumo yote inasomana na kuwa rafiki kwa mlipakodi.

Alisema kuwa kwa sasa serikali kupitia TRA imeweka mazingira wezeshi ambayo yanamsaidia mfanyabiashara kutoa risiti ya kielektroniki (EFD) ambayo kwa njia ya simu ya mkononi na ndiyo sababu ya mapato kuongezeka siku hadi siku.

**"Tumeanzisha huduma za bure ikiwamo namba za simu za bure zinazowezesha walipakodi kuwasiliana na ofisi za TRA na tumeanzisha ofisi zinazotembea (mobile tax offices) ambazo zitatumika kama ofisi kamili kwa ajili ya kutoa elimu ya kodi kwa umma na kusajili walipakodi wapya," alieleza Chande.**

# HADITHI

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo kuhupata kudhani.
Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana.
Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini.
Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa.
Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

# Malaika shetani-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




"Unakwenda kutafuta maisha mjini ndugu yangu?" Zuhura anauliza huku akijaribu kurejesha sauti yake tamu na laini. Lakini haikuwa kwenye ubora kama ule wa mwanzo. Walikuwa amesimama kweye eneo moja kijijini hapo, ambako Feruzi aliona hawezi kufuatiliwa na waliomtafuta. Ni sehemu ambayo yeye aliona ni salama zaidi. Na hiki pia kiliendelea kumtisha Zuhura, ambaye awali alijua ni eneo ambalo limekaa zaidi kitulivu kwa wawili wanaopendana wakikutana. "Hapana siendi mjini kusaka maisha." "Sasa?" "Naondoka hapa kwa ajili ya kuokoa roho yangu!" Ni jibu lililomtisha Zuhura. Kwa jinsi alivyomuona Faruzi. Awali alidhani kama ni mzaha, lakini kila akimuangalia, anaona ni mtu mwenye wasiwasi na anaongea kitu ambacho anamaanisha na si mzaha. "Kuna nini tena Faruzi mpenzi wangu?" Zuhura alimkumbatia mpenzi wake na akaanza kulia. "Usilie mpenzi. Usilie Zuhura. Wewe baki salama. Mungu akipenda nitarudi. Kuondoka kwangu hapa ndiyo usalama wangu. Kama nikikaa kwa siku moja tena mpaka kuingia kwa usiku wa kesho, sitakuwa hai. Nitaitwa marehemu. Sijui wewe, wazazi wangu, ndugu zangu mtakuwa kwenye hali gani. Kwa maana hiyo, ili niendelee kuwa hai. na nyinyi muendelee kuwa na mimi ni lazima niondoke." "Nani anataka kukutoa uhai, na tatizo ni nini mpenzi?" Akauliza kwa Zuhura kwa kwikwi. "Ni hadithi ndefu. Ila kwa sababu wewe ndiyo mpenzi wangu na msiri wangu mkubwa nitakwambia kabla sijaondoka. Nitakwambia kwa sababu moja tu. Ili usidhani labda nakumbia au kuna sababu yoyote mbaya ya mimi na wewe nyuma ya pazia. Nawajua nyinyi wanawake mawazi yenu." "Twende wote basi huko!" Zuhura akadakia. "Tungewenda wote. Na mimi ningependa sana. Lakini sina uhakika na ninakokwenda. Sipajui ninapokwenda, nakwenda kubahatisha tu. Siwezi kwenda kwa kubahatisha nikakuchua na wewe."

Zuhura akaanza kulia tena. Feruzi akapata kazi ya kumbembeleza. Aliponyamaza walitazamana kwa kuonekana huruma. "Niambie tatizo ni nini?" "Ni hivi, mimi sasa hivi natafutwa kuuawa. Na lengo na wauaji ni kuficha ushahidi. Kwa hiyo nataka nikusimulie wewe ili kama nisiporejea kabisa, basi kuwe na mtu mwingine ambaye atalifahamu. Nikamatwa kabla ya alfajiri muda wa kutoroka basi kuwe na mtu ambaye nimamuachia ushahidi ambao anaweza kwenda popote na kuuwasilisha.

Ila ninachokuomba ni kwamba, kwa sababu hili jambo kwa sasa liko moto usimuambie yoyote, mpaka pale litakapohitajika kwa muda muafaka na uwe na uhakika kuwa utalindwa na wanausalama, au mahakama." Zuhura hakusema kitu. Alibaki kumtazana Feruzi, alionekana kuwa na hamu ya kufahamu ni kitu gani kimetokea.

"Nilikuwa natoka kumuangalia rafiki yangu Sefu kijiji cha jirani. Nilipofika kwenye pori lile linalotenganisha na kijiji chetu, nikakutana na watu watatu ambao walionekana kama wanatana kufukia kitu. Waliponiona wakaacha zoezi lile na kuanza kunifukuza. Niliwazidi mbio hakunipata. Kutokana na tukio hilo mimi nilikaa kimya. sikumwambia mtu kitu chochote. Kesho yake ndiyo tukasikia kifo cha Naima. Na eneo ambalo amekutwa ndiyo lile lile nililowakuta wale jamaa. Ni mimi tu ndiyo nilijua nini nilifanyika pale. Nadhani wake jamaa walichokuwa wanataka pale ni kumfukia ili kupoteza ushahidi baada ya kumuua." Alichokuwa akiongea Faruzi kilimfanywa Zuhura kuingia ubaridi. Alihisi kama Feruzi anahadithia hekaya za kusadikika. Alihisi kama tumba linaanza kumsokota na kutaka kutapika kwa ajili ya hasira uliochangayikana na woga. "Unasema kweli Feruzi?" Aliuliza huku akimng'ang'ania akionekana ameingiwa na hofu.

"Unawajua Feruzi?" Zuhura akauliza swali lingine kabla ya kujibiwa la kwanza. "Nimeona kwa macho yangu. Na mimi kama wangenipata nimeokotwa maiti kama Naima, na nadhani wengi wangekuwa wanajiuliza ni kwa nini maiti za watu hawa wawili zimepatikana sehemu moja. Kwa nini wameuwa pamoja. Wengine wangedhani labda mimi ni mpenzi wake. Labda tumeuawa kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Yaani ninavyojua waswahili wangeongea mengi, kumbe mmoja ameuawa kwa sababu ya kuona mauaji wa mwingine alipokuwa anapita." "Sasa?" "Wale jamaa wanaonekana hawalali usingizi kwa sababu tayari kuna mtu amewaona. Na ionekana siyo wa kijiji hiki, lakini wametuma watu wa kijiji hiki ili wanifuatilie, ili wao waje kunimaliza. Kwa maana hiyo kama nilivyokwambia muda wowote naweza kuuawa." Zuhura hakusema kitu tena, alibaki kumtazama Feruzi kwa huruma wakati mwingine kumwaga machozi. "Usilie, Mungu akipenda nitarudi. nadhani nimeshakwambia hilo. Kaa nalo. Ni siri ya tari sana, usimwambie mtu. Ngoja kuna wakati wake. Mimi kama nilifanikiwa kurejea tutaoana. Twende nikusindikize nyumbani ili na mimi nianze kujiandaa. Zuhura aligoma "Nitakwenda mwenyewe, rudi nyumbani kwa usalama wako." Zuhura sasa alianza kuwa mwalimu wa Feruzi, wakati mwanzo alimuona kama mlaghai. "Hapana. Wewe ni mpenzi wangu, kama wataniua mbele yako sawa." Alimjibu huku akimshika mkono na kuanza kumsindikiza kwao. Walipofika hatua kadhaa kabla ya kufika nyumbani, waliagana na kukumbatiana na mabusu moto moto "Mungu akulinde mpenzi wangu huko uendako. Akitangulie na mabaya yote, urejee mapema tuoane. Enhee kwanza nimesahau." "Umesahau nini Zuhura tena?" "Utarudi wakati gani? Na utajiaje kama huku mambo yamepoa? Na wanaokutafuta unadhani hata ukikaa miaka mitatu ukirudi ndiyo wataacha kukumaliza kama watakuwepo?" "Da! Umeuliza swali zuri kweli mpenzi wangu. Sikutegemea swali kama hili. Ni kwamba mimi nakwenda huko. Lakini nikifika nitatafuta mtu yoyote au mwanausalama, polisi ambaye atakuwa tayari kunisikiliza kwa hili linalolisema ili aje kulimaliza huku. Kuwakamata wote waliohusika. Hapo ndipo nitakaporudi." "Unadhani ni rahisi kiasi hicho?" "Si rahisi, lakini ninajitahidi." "Basi sana, nitafurahi kwa sababu mimi Naima alikuwa shoga yangu mkubwa, nimehuzunika sana na kifo chake." Waliagana. Ilikuwa ngumu kidogo kuachana, lakini ilikuwa lazima waachane. Feruzi alisubiri hadi Zuhura alipofunga mlango. Haikuwa rahisi, kwani Zuhura alichelewa kuufunga kutokana na kutaka tu kumuona Feruzi agalau kwa mara ya mwisho, kwani alitarajia kuwa atamuona tena baada ya muda mrefu kupita, au asimuone tena.

Wakati anarejea, Feruzi alihisi kama kuna watu wanamfuata kwa nyuma.

> **"Wale jamaa wanaonekana hawalali usingizi kwa sababu tayari kuna mtu amewaona. Na ionekana siyo wa kijiji hiki, lakini wametuma watu wa kijiji hiki ili wanifuatilie, ili wao waje kunimaliza. Kwa maana hiyo kama nilivyokwambia...**

*Itaendelea Jumamosi*

# AZAM YATAMBA KUIMARIKA, NDOTO ZA UBINGWA KUTIMIA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Azam FC ikifichua ilikuwa ina mpango wa kwenda Qatar kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, inajivunia mechi saba za kirafiki walizocheza mpaka sasa ambazo zimewafanya wawe tayari kwa mapambano wa hatua ya lala salama.

Azam ililazimika kubadilisha mpango wa safari hiyo ya ughaibuni kutokana na ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara kurudishwa nyuma kutokana na kusogezwa mbele kwa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema kipindi hiki cha mapumziko ya tangu Desemba, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rachid Taoussi, amekuwa na kikosi chake kwa muda mrefu kuwaangalia wachezaji wapya waliosajiliwa dirisha dogo ili kuwaunganisha.

Ibwe alisema pia kocha alipata nafasi ya kuwatumia katika mechi za kirafiki nyota ambao hawakuwa wakipata namba katika kikosi cha kwanza ili kuboresha viwango vyao.

„Tulikuwa na safari ya kwenda Qatar, lakini kurudishwa nyuma ligi kumetufanya kuahirisha safari hiyo na kuendelea na mazoezi hapa hapa. Tumecheza jumla ya mechi saba za kirafiki, nne hazikuwa na wazi, tatu zilikuwa rasmi na mashabiki waliruhusiwa kuangalia, baadhi ni dhidi ya Mtibwa Sugar tulichezea Manungu Complex, nyingine tulicheza dhidi ya JKT Tanzania, Meja Jenerali Isamuhyo.

Katika michezo hii, kocha amepata nafasi ya kuwaona wachezaji wapya ambao hajawahi kuwatazama kabla ya hapo, na wale ambao hawakuwa wakipata nafasi ya kuanza kwenye michezo mingine, kusema kweli imetusaidia sana na sasa tupo tayari kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu,“ alisema Ibwe.

Aliongeza malengo yao msimu huu hayabadilika ni kama yale ya msimu uliopita, nayo ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

„Tupo ndani ya malengo, mipango yetu ni ile ile, tunataka ubingwa wa Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho, tukishindwa sana basi tuwe hata wa pili,“ Ibwe aliongeza.

Azam yenye pointi 36 itashuka kwenye Uwanja wake wa nyumbani, Azam Complex, Dar es Salaam Februari 6, mwaka huu kuwakaribisha KMC.

Simba yenye pointi 40 inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 39.



Beki wa kushoto wa Yanga Princess, Diana Mnally akimiliki mpira katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Alliance Girls iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. Yanga ilishinda mabao 4-1. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Stand United yafufua matumaini

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa kwanza wa mabao 3-1 dhidi ya Kiluvya FC, Stand United ya mkoani Shinyanga, imetangaza hali ya hatari katika mzunguko wa pili wa Ligi ya Championship.

Katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Kambarage, mabao ya washindi yalifungwa na Lucas Sendama, Adam Uledi na Omari Khamis, aliyefunga dakika za majeruhi.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kufikisha mabao 32, ikiwa katika nafasi ya nne, nyuma ya Geita Gold ambayo ipo nafasi ya tatu kwa tofauti ya pointi moja tu.

Wakati ligi hiyo ikiwa imefikisha raundi ya 16, Mtibwa Sugar bado imeendelea kung'ang'ania kileleni ikiwa na pointi 41, Mbeya City nafasi ya pili na pointi zake 34 ikifuatiwa na Geita Gold yenye pointi 33.

Katika michezo mingine kwenye uwanja mbalimbali, Bigman, ikiwa, Uwanja wa Ilulu, Lindi, iliitwanga Mbeya City bao 1-0, Transit Camp, ikipata kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Biashara United, mechi ikichezwa, Uwanja wa Mabatini, Mlandizi, Pwani.

Hata hivyo, ushindi huo bado umeifanya kuendelea kukamata mkia, ikifikisha pointi nne.

Timu mbili zitakazomaliza juu zitapanda moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

# KenGold: Tutabakia Ligi Kuu msimu ujao

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 4-1 katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Real Nakonde ya Zambia, Kocha Mkuu wa KenGold FC, Vladislav Heric, amesema atahakikisha wanapambana na kubakia katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabao ya KenGold katika mechi hiyo ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, sambamba na utambulisho wa wachezaji wapya yalifungwa na Erick Kabamba, Maulid Mbegu, George Sangija na Komanje Sandale.

Kocha huyo alisema kikosi chake kimeanza kuimarika tofauti na kilivyokuwa wakati anajiunga na timu hiyo, hivyo anaamini watarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa imara.

Alisema anafahamu kila timu imejiimarisha, lakini mabadiliko yaliyofanyika katika kikosi chake yatasaidia kuiondoa timu hiyo kwenye janga la kushuka daraja.

„Kikosi changu kimebadilika sana, kimeanza kuwa na muunganiko, wachezaji wameanza kuelewana, tunaamini tutakuwa na matokeo tofauti na timu ilivyokuwa katika mzunguko wa kwanza, tuko tayari kwa ajili ya kuipeperusha vyema bendera ya timu,“ alisema kocha huyo.

Aliongeza hatua ya pili huwa ngumu katika ligi zote kwa sababu timu zote zinaingia ili kutimiza malengo yake na kubwa ni kutwaa ubingwa au kujinusuru na kushuka daraja.

„Najua moja ya sababu kubwa ya mimi kujiunga na timu hii ni kuhakikisha inafanya vizuri katika ligi, kuleta mabadiliko, ninafurahi kuona sehemu ya mapendekezo yangu yalifanyiwa kazi na sasa tuna kikosi kinachoweza kutoa ushindani,“ aliongeza kocha huyo raia wa Serbia.

Mtihani wa kwanza wa kocha huyo utakuwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 5, mwaka huu watakapowafuata mabingwa watetezi, Yanga kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

KenGold yenye pointi sita ikiwa imecheza michezo 16, inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo ambayo vinara ni Simba yenye pointi 40 wakifuatiwa na Yanga yenye pointi 39.

Ligi hiyo inarejea rasmi kuanzia kesho kwa Yanga kuwakaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa KMC Complex huku kesho Simba itashuka ugenini kuwavaa wenyeji Tabora United.

## ZISIKUPITE

### TEL AKARIBIA BAYERN
KLABU ya Tottenham Hotspur imekubali mkataba wa pauni milioni 50 na Bayern Munich kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Mathys Tel, mwenye umri wa miaka 19. ***(L'Equipe)***

### UNITED YAMTAKA TEL
MANCHESTER United inalenga kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya Argentina mwenye umri wa miaka 20, Alejandro Garnacho, na kumtaka pia nyota Mfaransa, Mathys Tel kwa mkopo. ***(Independent}***

### MITOMA ANUKIA SAUDIA
KLABU ya Al-Nassr inapanga kutoa ofa ya pili na ya mwisho kwa winga wa Brighton na Timu ya Taifa ya Japan, Kaoru Mitoma, mwenye umri wa miaka 27 yenye thamani ya pauni milioni 90. ***(CBS Sports)***

### ARSENAL YAMBANIA TIERNEY
ARSENAL wamemzuia beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 27 kuelekea Celtic msimu ujao. ***(Telegraph)***

### ASENSIO AIVUTIA PSG
MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 29, ni mmoja wa wachezaji washambuliaji ambao Aston Villa wanavutiwa kuwasajili kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Mail)***

### WATKINS NJIA MOJA
MSHAMBULIAJI wa England, Ollie Watkins, atakuwa tayari kujiunga na Arsenal mwezi huu, lakini Aston Villa wamedhamiria kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Mail)***

### EMERY AMTAKA FELIX
KIUNGO wa kati wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 25, analengwa na Kocha wa Aston Villa, Unai Emery. ***(Express)***

### RODRYGO KUMRITHI NEYMAR
KLABU ya Al-Hilal imetoa ofa kubwa kwa winga wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa mshambuliaji wa Brazil, Neymar (32). ***(Marca)***

### HENDERSON SOKONI
KLABU ya Monaco inakamribia kuafikiana na Ajax kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa England, Jordan Henderson, mwenye umri wa miaka 34. ***(Fabrizio Romano)***

### FERGUSON ANUKIA EVERTON
KLABU ya Everton inatathmini dau la kuchelewa la kumnunua mshambuliaji wa Brighton mwenye umri wa miaka 20 na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson. ***(i Sport)***

### CHELSEA YAMTAKA KOBEL
CHELSEA inavutiwa na mlinda lango wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Uswizi, Gregor Kobel mwenye umri wa miaka 27, ingawa kuna uwezekano wa kuhama msimu wa joto. ***(Independent)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AMORIM: TUNAUTAKA UBINGWA WA UEFA

●●● Kocha huyo asema United ina uwezo wa kubeba taji hilo kwa...

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim amesisitiza licha ya mwanzo wake mgumu kama kocha wa Manchester United, timu yake lazima ilenge kushinda taji la Ligi ya Europa baada ya kutinga hatua ya 16 bora baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Steaua Bucharest juzi.

Amorim alikuwa kocha wa kwanza wa United kupoteza michezo mitano kati ya 10 ya kwanza katika mashindano yote tangu Walter Crickmer mwaka 1932, lakini maboresho ya hivi karibuni yamemsaidia kuzoea maisha pale Manchester.

Mreno huyo alikiri baada ya ushindi wa Jumapili dhidi ya Fulham, anahisi kama ana miaka 10 tangu alipotua Old Trafford Novemba, mwaka jana kumrithi, Erik ten Hag.

"Sioni tofauti kubwa jinsi tunavyocheza, lakini leo (juzi) tulikuwa na wakati mwingi wa kufikiria na sasa unaweza kuona mwenendo, wazo lipo kwa sababu tuna muda mwingi wa kucheza na kuelewa mchezo," alisema Amorim akiwaambia waandishi wa habari.

"Nadhani tunaweza kwenda mchezo kwa mchezo na tunaweza kushinda. Kisha una jukumu, bila kujali mazingira, uko Manchester United kwa hiyo lazima upigane kushinda mataji.


"Unapofika katika hatua hii ya mashindano yoyote, chochote kinawezekana na wanaweza kuthibitisha wanaweza kushinda dhidi ya mtu yeyote."

Kumaliza kwa United katika nafasi ya tatu katika awamu ya kwanza ya Ligi ya Europa kulihakikisha wanaepuka mchujo wa michezo miwili na kufika hatua ya 16 bora.

"Hilo ni muhimu sana kwetu, kuwa na muda wa kufanya mazoezi, kujenga uhusiano kati ya kila mtu, wafanyakazi, kila mtu aliyepo kwenye mazoezi, kwenda uwanjani, kujuana katika mazingira yanayofaa," aliongeza Amorim.

„Basi tuna wiki moja ya kujiandaa na mchezo, mwanzoni mwa wiki unaweza kufanyia kazi wazo lako kisha ukapata muda wa kuandaa mchezo na kumlenga mpinzani. Naweza kuwaelewa vizuri wachezaji wangu."

# De Bruyne kupewa mkataba mpya City




**MANCHESTER, England**

KEVIN De Bruyne anatumaini kumaliza sintofahamu juu ya mustakabali wake wa Manchester City kwa kusaini mkataba mpya wa kubakia kwenye Uwanja wa Etihad, kwa mujibu wa ripoti.

De Bruyne ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na, anapojiandaa kutimiza umri wa miaka 34 ifikapo Juni, anapendekezwa kuondoka Man City na kuelekea Saudi Arabia.

Hata hivyo, gazeti la The Times limesema De Bruyne anatarajia kusaini mkataba mpya na City.

Jambo la msingi katika uamuzi wa De Bruyne ni furaha ya familia yake na matumaini yake ya kuiwakilisha Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia la mwaka 2026.

Kocha wa City, Pep Guardiola hajaficha nia yake ya kuendelea kufanya kazi na De Bruyne, na amekiri hadharani ukweli kiungo huyo hayupo tena katika ubora wake.

Majeraha yamemwathiri sana De Bruyne katika miaka ya hivi karibuni na yamemfanya acheze mechi 11 pekee za Ligi Kuu ya England hadi sasa msimu huu.

***

# Ancelotti akosoa muundo wa UEFA

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amekosoa muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu baada ya toleo la kwanza la awamu ya ligi kumalizika wiki hii.

Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), limerekebisha mashindano hayo msimu huu, na kufutilia mbali hatua ya makundi kwa kupendelea jedwali moja la ligi na kuongeza idadi ya mechi za kabla ya mtoano kutoka timu sita hadi nane.

"Mechi nyingi sana," lilikuwa ni jibu la Ancelotti kwa waandishi wa habari Jumatano usiku alipoulizwa tathmini yake juu ya muundo mpya wa awamu ya ligi.

"Kumekuwa na mechi nyingi sana, lakini kwa kila mtu," alisema.

"Na kwa wakati huu katika soka, tunapaswa kuondoa mechi, sio kuongeza zaidi. Hayo ni maoni yangu."

Katika misimu iliyopita, timu mbili za juu katika kila kundi zilifuzu kwa hatua ya 16 bora.

Lakini kwa sasa ni timu nane tu za juu katika awamu ya ligi ndizo zilizohakikishiwa nafasi katika raundi hiyo.

Washindi 16 wanaofuata, ambao wanajumuisha Madrid baada ya matokeo kadhaa ya kukatisha tamaa, lazima kwanza waende kwenye mchujo wa mechi mbili za kufuzu.

Ili kufika fainali tena msimu huu, Madrid italazimika kucheza mara nne zaidi ya ilivyokuwa msimu wa 2023/24.

Fainali hiyo itakuwa ni mchezo wa 17 wa Ligi ya Mabingwa kwao msimu huu, ikilinganishwa na mechi 13 msimu uliopita.



# CHIESA: NINATAKA KUBAKI LIVERPOOL




**LIVERPOOL, England**

WINGA wa Liverpool, Federico Chiesa, amezungumzia mustakabali wake katika klabu hiyo, baada ya hivi karibuni kuhusishwa na mpango wa kuondoka baada ya kuanza maisha kwa changamoto pale Anfield.

Chiesa alitajwa kama moja ya dili za msimu wa joto wakati michuano ya Euro 2020 alipowasili kutoka Juventus kwa bei iliyopunguzwa yenye thamani isiyozidi pauni milioni 10.

Lakini kutokana na kuwa majeruhi, pamoja na ushindani mkali wa nafasi, muda wa mchezo umekuwa karibu kutowezekana.

Kabla ya wiki hii, Chiesa alikuwa amecheza kwa dakika 190 pekee akiwa na jezi ya Liverpool, huku akihusishwa na kutaka kuelekea Napoli dirisha la Januari.

Kichapo cha Liverpool katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka kwa PSV Eindhoven Jumatano iliyopita ilikuwa ni mara ya pili kwa Chiesa kuanza kwa Liverpool, na mara ya kwanza tangu Septemba, mwaka jana.

Na ingawa mchezo haukuisha jinsi timu ingetaka, ilitoa motisha ya kutosha kwa Chiesa kutangaza wazi nia yake ya kubaki.

"Lazima nimshukuru kocha, wafanyakazi, kwa kunipa uwezekano wa kucheza dakika 90," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwangu ilikuwa nzuri, nilihitaji. Tangu nijiunge na Liverpool nilitaka kujidhihirisha, sikuweza kwa sababu nyingi. Dakika 90 baada ya muda ilikuwa nzuri kwa hiyo sina budi kumshukuru kocha.

"Kuna nafasi ya kuimarika, kuwa bora na bora na kuwa katika kiwango bora zaidi cha mchezo wangu. Lakini tuna timu kubwa na ni ngumu kucheza, hiyo ni kawaida. Nataka kuwa hapa, nataka kuichezea Liverpool, nataka kujipa changamoto na nitakuwa tayari kwa nafasi yangu ijayo."

# SINGIDA BLACK STARS YAREJEA NYUMBANI, YAITISHA KAGERA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI hatima ya nyota wake watatu waliopewa uraia wa Tanzania ikiwa bado chini ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), kikosi cha Singida Black Stars kimerejea mkoani, Singida tayari kuisubiri Kagera Sugar, imeelezwa.

Singida Black Stars iliweka kambi jijini Arusha lakini imelazimika kuvunja kambi hiyo kutokana na mabadiliko ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajia kurejea tena kuanzia leo.

Matajiri hao wa asali wataikaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Liti, huku uongozi wakisema wachezaji wote waliosajiliwa dirisha dogo wamekamilisha taratibu za usajili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, amesema licha ya uchovu wa safari, kikosi chao kilichoko chini ya Kocha Mkuu, Hamdi Miloud, mwenye uraia pacha wa Algeria na Ufaransa, kiko tayari kwa mzunguko wa pili.

"Tumewasili nyumbani baada ya kukaa kambi ya majuma kama matatu hivi, wachezaji wamechoka sana kwa hiyo tunawapa mapumziko mafupi, wamefanya kazi kubwa sana kule Arusha kujiandaa, watapumzika kwa siku mbili, baada ya hapo tutarudi kwenye uwanja wa mazoezi, tunajiandaa na mchezo wa Ligi Kuu, tutacheza na Kagera Sugar hapa hapa," alisema Massanza.

Alisema katika mchezo huo, Singida Black Stars itaanza kuwatumia wachezaji wao wapya endapo kocha ataona inafaa kwa sababu wamekamilisha kila kitu, ikiwamo vibali na leseni.

"Niwaambie tu mashabiki wa Singida wachezaji wetu wote waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili, wote wapo tayari kucheza, hawana shida ya vibali wala leseni na hata wale Watanzania wenzetu mambo ni shwari, kwa hiyo hakuna kisingizio, wala msiwe na ‚stress', waombeeni sana wachezaji wetu maana vita imekuwa kubwa," alisema ofisa huyo.

Nyota wa Singida Black Stars ambao wamepewa uraia wa Tanzania ni pamoja na Josephat Arthur Bada, Emmanuel Keyekeh na Mohammed Domaro Camara.

Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, ilifanya kikao chake juzi na moja ya mashauri ni mchakato kuhusu nyota hao kupewa uraia wa Tanzania.



Wasanii wa ngoma ya asili ya Kisukuma wakicheza wakati wa Mkutano wa Nishati wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kipanga FC, New City dimbani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kipanga FC inatarajia kuikabili New City FC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau, visiwani hapa.

Kocha Mkuu wa Kipanga FC, Hassan Khamis, aliliambia gazeti hili anatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu kwa pande zote mbili.

Khamis alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa umakini na utulivu kwa sababu kwa sasa wanahitaji zaidi pointi tatu ili kujiondoa katika nafasi waliyoko kwenye msimamo wa ligi hiyo.

„Hatutaki kufanya makosa katika mchezo huu wa kwanza katika mzunguko wa pili, ninawakumbusha wachezaji kukifanya kile tunachokifanya kwenye uwanja wa mazoezi. Tumefanya maboresho mengi katika kipindi chote cha mapumziko ya ligi, tumefanikiwa pia kupata maingizo mapya kulingana na mahitaji yetu," alisema kocha huyo.

Aidha alisema katika mchezo huo anatarajia kuwatumia wachezaji watano wapya ambao wamejiunga na timu hiyo wakati wa dirisha dogo la usajili ambao anaamini watakiongezea nguvu kikosi chao.

Kipanga FC yenye pointi 17 inateremka uwanjani ikiwa ipo katika nafasi ya 12 na wakati wapinzani wao New City wenye pointi 12 wako nafasi ya 14 katika msimamo wa hiyo ya juu Zanzibar.

## Simba: Tunakwenda Tabora kulipiza kisasi

INATOKA UK. 24

Azam FC mabao 2-1, nyumbani kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Simba itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi mnono wa mabao 4-0, katika mechi ya mzunguko wa pili msimu uliopita, shukrani ziende kwa Pa Omar Jobe, Sadio Kanoute, Che Malone Fondoh na Fred Koublan, kwa kupachika wavuni magoli.

Ikumbukwe vinara hao walipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United, katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Agosti 17, mwaka jana kwenye Uwanja wa KMC Complex, Che Malone, Valentino Mashaka na Awesu Awesu, wakifunga.

Rekodi pia zinaonyesha kuwa msimu huu, Simba haijapoteza mechi yoyote ya Ligi Kuu, ikicheza ugenini, badala yake imeshinda zote, huku sare moja ya mabao 2-2 iliyoipata dhidi ya Coastal Union na kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga, vyote ilikuwa kwenye michezo yake ya nyumbani.

## Yanga yawaahidi furaha mashabiki

INATOKA UK. 24

"Tunakutana na Kagera Sugar... nafahamu na wao wamekuja kujaribu kupata ushindi, hautakuwa mchezo mwepesi lakini ni lazima tupate ushindi, tuna michezo 15 ya mzunguko wa pili, malengo yetu ni kushinda yote, tunataka kutetea ubingwa wetu," alisema Ramovic.

Kocha huyo alisema pia kuelekea mchezo huo, wachezaji wake wote wapo katika morali kubwa na wanafahamu umuhimu wa kupata pointi tatu.

„Tukipoteza mchezo huu utaanza kutuweka katika wakati mgumu, mzunguko huu wa pili si wa kupoteza ovyo mechi, ni mzunguko ambao ukifanya makosa wenzako watayatumia vizuri ili kusonga mbele," Ramovic alisema.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Ali Kamwe, alisema kikosi chao kiko tayari kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki na wanachama wao.

Kamwe amewataka mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi kuwashangilia wachezaji wao ili wakamilishe kile wanachotarajia kukipata katika mechi hiyo.

"Njooni kwa wingi katika mechi ya kesho (leo), tunaenda kuanza rasmi safari yetu ya kutetea ubingwa, hatutaki kufanya makosa, tumerejea katika mashindano yetu, huku sisi ndio bora zaidi," Kamwe alitamba.

Wakati huo huo, mabosi wa Kagera Sugar, wamesema wamekuja Dar es Salaam kufuata pointi tatu na hawataingia uwanjani kinyonge.

Mtendaji Mkuu wa Kagera Sugar, Thabit Kandoro, alisema wamejiandaa vizuri kwa mchezo huo na hawana ‚ugeni' na uwanja wa KMC ambao utakaotumika leo.

"Hatutaingia kinyonge, tunawaheshimu Yanga kama moja ya timu kubwa, lakini ndani ya uwanja tutakuwa sawa," alisema Kandoro.

Aidha, kocha wa timu hiyo, Melis Medo, amesema wamejiandaa vyema kuelekea mechi hiyo na ameandaa mfumo ambao unaweza ukawapa matokeo mazuri.

Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea tena kesho kwa Tabora United kuikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Michezo

Jumamosi Februari 1, 2025

Nipashe

## Amorim: Tunautaka ubingwa wa UEFA

UKURASA 21





Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kushoto), akijiandaa kumtoka beki kisiki wa timu hiyo, Ibrahim Hamad 'Bacca' katika mazoezi kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yawaahidi furaha mashabiki

## ●●●Yaitangazia hatari Kagera, yafunguka ina mechi 15 za 'jasho na damu'...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI inatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, benchi la ufundi la Yanga limesema wana michezo 15 ya ‚ulazima wa kushinda' ili kuhakikisha wanatetea ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

Ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi inaonyesha mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Yanga yenye pointi 39 iko kwenye nafasi ya pili, nyuma ya vinara, Simba yenye pointi 40, Azam FC inafuatia ikiwa na pointi 36 huku Kagera Sugar yenye pointi 11 iko nafasi ya pili kutoka mkiani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Saed Ramovic, amesema kwa kuanzia wanataka kupata ushindi katika mchezo wa leo ili kujiongezea hamasa ya kufikia malengo.

Ramovic alisema wameingia katika mzunguko wa pili ambao wanaamini hautakuwa mwepesi kwa sababu kila timu itataka kupambana kupata ushindi ili kufahamu nafasi watakayomaliza baada ya msimu kumalizika.

INAENDELEA UK. 23

## Simba: Tunakwenda Tabora kulipiza kisasi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajiwa kuwasili Tabora mapema leo, uongozi wa timu hiyo umesema umekwenda mkoani humo kwa lengo moja la ‚kulipiza kisasi' kufuatia wenyeji Tabora United kuzifunga timu nyingine za Dar es Salaam walipokutana katika mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Tabora United inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema mbali na kuhitaji ushindi, ‚kuzilipia' kisasi timu zote za Dar es Salaam ni moja ya kilichowapeleka Tabora.

Ahmed alisema hawahofii chochote kuelekea mchezo huo, badala yake wamedhamiria kuchukua pointi tatu muhimu na kujiimarisha kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Kwanza tunakwenda kuzilipia kisasi timu zote za Dar es Salaam ambazo zimeonewa na Tabora United, haiwezikani timu ya Dar es Salaam ikafanywa mnyonge, kwa hiyo tunakwenda kumlipia kila Mwana-Dar es Salaam ambaye alidhuriwa katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu. Ni jukumu la timu zote kutuunga mkono, kukaa nyuma yetu ili tumshikishe adabu," alisema Ahmed.

Aliongeza mchezo huo hautakuwa rahisi kutokana na Tabora United kujiamini, lakini wao pia wanamatumaini kutokana na ubora wa kikosi cha benchi lao la ufundi kiinachoongozwa na Kocha Mkuu, Fadlu Davids.

"Haitakuwa mechi rahisi, ni ngumu kwa sababu Tabora United inaonekana baada ya kupata ushindi dhidi ya timu za Dar es Salaam, imejenga kujiamini sana, tuseme pia ni timu nzuri, lakini amezifunga timu anazofanana nazo.

Uwezo wake wa kupata ushindi ni kwa timu inayoshika nafasi ya pili kushuka chini, kuna baadhi ya watu wanasema eti tunakwenda kucheza ugenini sisi hatuna ugeni, kumbuka msimu uliopita pale pale tuliwakung'uta mabao 4-0, popote sisi tunakanyaga na popote kambi," Ahmed alitamba.

Tabora United iliifunga Yanga mabao 3-1, mechi iliyochezwa Novemba 7, mwaka jana kwenye Uwanja wa Azam Complex halafu ikapata ushindi mwingine wa ugenini magoli 2-0 dhidi ya KMC na Desemba 13, mwaka jana ikawachapa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >